# Nipashe

Jumamosi Januari 28, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581204

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11


SUPA JACKPOT
TZS. 1,069,861,169
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




**MCHECHU:** NHC imepata 'wazimu' kuendeleza miradi

UKURASA 3

BIMA AFYA KWA WOTE

# Viongozi dini wataka ruzuku kutibu maskini

UK. 2



Askofu Dk. Fredrick Shoo

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu



Waombolezaji wakitoa heshima za mwisho kwa mwili wa mwanafunzi wa Kitanzania, Nemes Tarimo, aliyefariki dunia vitani Ukraine, ulipowasili nyumbani kwao, Mbezi kwa Msuguri, Dar es Salaam jana. Nemes alijiunga na kikundi cha kijeshi cha Russia kiitwacho Wagner kwa ahadi ya kulipwa fedha na kuachiwa huru baada ya vita kutokana na kifungo chake cha miaka saba jela. **PICHA: MIRAJI MSALA**

UKURASA WA 3

## FISI WA AJABU ANG'ANG'ANIA ZIZINI



KATIKA hali isiyokuwa ya kawaida, fisi anayedaiwa wa ajabu amekang'ang'ania kwenye zizi la mifugo na kuzua taharuki kwa wakazi wa Kitongoji cha Mwamatome kijijini Nyakato, Kata ya Tabaruka wilayani Sengerema mkoani Mwanza...

# Utapeli mpya watumishi waliotimuliwa vyeti feki

UKURASA 3

# Viongozi SACCOS kikaangoni kwa madai kutafuna fedha za walimu

UKURASA 8


MICHEZO LAZIMA TUWACHAPE UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde (kushoto), akikagua shehena ya mbolea kabla ya kusafirishwa kwenda Mkoa wa Rukwa, wakati wa uzinduzi wa kuanza kwa usambazaji wa mbolea kupitia Kampuni ya Mbolea Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kushoto ni Meneja Mkuu wa kampuni hiyo, Samuel Mshote. **PICHA: MOSHI LUSONZO**

# Viongozi wa dini wataka ruzuku matibabu maskini

**Na Maulid Mmbaga**

VIONGOZI wa dini wametoa maoni mbalimbali kuhusu maboresha ya Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ikiwamo kutolewa ruzuku itakayotumika kuwasaidia wananchi wenye kipato cha chini ambao hawataweza kumudu gharama zilizowekwa.

Jana mkoani Dar es Salaam, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alikutana na viongozi wa dini kutoka mikoa 27 kwa lengo la kujadili kuhusu muswada huo.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Askofu Dk. Frederick Shoo, alipowasilisha maoni ya jumuiya hiyo, alishauri kipato kutoka Sekta ya Madini pekee kinaweza kuwafadhili wananchi ambao ni maskini kabisa na hawawezi kujilipia gharama za bima.

Alisema inapoguswa afya, ni suala la jumla linalogusa afya ya akili na mwili, akifafanua kuwa kuwa likizingatiwa vizuri, litaakisi katika kutoa tafsiri ya maendeleo ya jumla ya kielimu, uzalishaji na uchumi.

"Muswada haujaweka bayana hatua zitakazochukuliwa kwa skimu ya bima ya afya endapo utaratibu wa kulipa gharama utakiukwa. Sisi tulipendekeza kuwe na faini kwa asilimia tano mpaka 15 ya thamani ya ongezeko la fedha kwa skimu za bima ya afya zitakazochelewesha malipo kwa vituo vitavyotoa huduma kwa kipindi cha siku 90 na kuendelea," alisema Askofu Shoo.

Pia alipendekeza kuwe na uhuru kwa watu wote wakiwamo watumishi wa umma kuruhusiwa kuwa wanachama wa skimu ya bima watakayopenda badala ya kuwa wanachama wa Bima ya Afya kwa Umma kisheria, akidai kuwa hatua hiyo itasaidia kuboresha ubora wa skimu za bima kiushindani.

"Sisi tupo pamoja na tutaendelea kutoa elimu kwa waumini wetu, na nitoe ujumbe kwa viongozi wenzangu wa dini, tuchukue nafasi yetu kuendelea kuelimisha watu," alisema Askofu Shoo.

Mwakilishi wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Hassan Chizenga, alishauri muswada huo usijumuishwe na skimu za bima nyingine kama za magari na nyumba na kwamba uwe unajitegemea na kusimamiwa kwa upekee na Wizara ya Afya.

Alisema mkakati huo wa Bima ya Afya kwa Wote waamini utaboresha huduma ya afya kwa wananchi wote, akibainisha kwamba wanatambua jamii ya Watanzania kutokana na uchumi wao kuwa mdogo, inapata shida pindi wanapopatwa na changamoto za kiafya.

"Sisi viongozi wa dini tunaamini kwamba waumini wetu wakiwa na afya njema watakuwa na mchango mkubwa katika ibada na hata uchumi, hivyo tunaipongeza serikali kwa jitihada hizi za kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora za kimatibabu," alisema Chizenga.

Mwakilishi kutoka Baraza la Makanisa ya Pentekosti Tanzania (CPCT), Ezra Msanya, alisema suala la afya ni nyeti na muswada huo umekuja kwa wakati sahihi, akibainisha kuwa wananchi wanapolalamika ugumu wa maisha, ugumu huo unaongezeka endapo hatakuwa na afya njema kwa sababu hawatoweza kufanya shughuli yoyote ya kukabiliana na ugumu wa maisha.

Waziri Ummy aliwahakikishia kuwa itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za makusudi ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya na kwamba dhana ya Bima ya Afya kwa Wote inashikamana moja kwa moja na ubora wa huduma za afya, hasa kwenye vituo vinavyosimamiwa na serikali.

Alisema amefurahishwa na maoni na michango iliyotolewa na viongozi hao wa dini, akiahidi watatumia vipande vya baadhi ya maelezo yaliyotolewa ili kuwahamasisha na kuwaelimisha zaidi wananchi kuhusu umuhimu wa bima ya afya katika maisha yao.

Vilevile, aliwahakikishia viongozi wa dini kwamba wananchi wanapata huduma bora za afya kupitia bima na kuwaelimisha, akibainisha kuwa Watanzania wengi ni wazito katika kuwekeza kwenye afya zao na wanasubiri waugue ndipo waende kuhangaika kutafuta fedha za matibabu.

"Kwa sababu hili suala linakwenda kwa hatua, tuliona tupunguze baadhi ya masharti ili watu wajiunge kwenye huduma ya afya kwa hiari, lengo letu tunatamani kila Mtanzania ajiunge na bima ya afya, ili kuwezesha makundi yote kupata huduma bora za afya.

"Huu ni mwaka wangu wa sita katika sekta ya afya, ninaona ni kwa kiasi gani watu wanaingia kwenye umaskini pale wanapouguza au wenyewe kuugua, watu wanauza mali zao ili kupata fedha za matibabu yao au ya ndugu," alisema Ummy.

# Samia aadhimisha 'bethidei' kwa staili yake

**Na Romana Mallya**

WAKATI Rais Samia Suluhu Hassan akisherehekea siku yake ya kuzaliwa jana kwa kutoa misaada katika vituo saba vya watoto yatima, wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya wameungana naye kwa kufanya hafla maalum ya kumpongeza na kukata keki yenye ujumbe maalum.

Rais wa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya, Saruni Jessy, akizungumza kwa niaba ya wenzake katika hafla fupi waliyoiandaa nchini Kenya, sambamba na ukataji wa keki maalum waliyoiandaa, alitaja sababu iliyowasukuma kufanya hivyo.

"Mama tunakupenda wewe ndiye Rais wa kwanza mwanamke Afrika Mashariki. Tunakupenda tunakutakia kila la keri vile ambavyo umeweza kuleta upendo Afrika Mashariki. Tunaomba uendelee hivyo," alisema Rais huyo huku akinukuu ujumbe maalum uliomo kwenye keki hiyo.

"Happy Birthday Mama Samia Suluhu, wewe ndiye mama East Africa nzima. Tunakupenda na tunakuombea uzima, sisi viongozi wa vyuo vikuu Kenya nzima, tukifurahia uongozi wa baba yetu Ruto (Rais wa Kenya, William Ruto). Tunasema tunakutambua kama mama yetu.

"Mama ukihudumia Watanzania kumbuka pia una watoto huku Kenya na East Africa, siku ya leo tunakuhakikishia tutazidi kukupa support kama wanafunzi wa Afrika Mashariki, tungependa tupatane tujadiliane tuinue Afrika Mashariki na tujisikie karibu nawe mama.

"Kwa hii siku yako ya kuzaliwa, tunakutakia kheri njema, furaha, afya nzuri na maisha marefu, kwa siku zote tunasema, mama ndiyo best," ulisomeka ujumbe huo.

Baada ya kusoma maelezo hayo, wanafunzi hao waliungana kwa pamoja na kukata keki kama sehemu ya kusherehekea siku ya kuzaliwa kwa Rais Samia.

Wakati wanafunzi hao wakimpongeza Rais Samia, jana Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, kwa niaba yake, alikabidhi vitu mbalimbali pamoja na fedha taslimu kwa vituo vya watoto vilivyotolewa na Rais.

Makabidhiano hayo yalifanyika katika kituo cha watoto kijulikanacho kama Children's Home, Msimbazi, Ilala jijini Dar es Salaam na Kituo cha Watoto cha Mburahati. Vingine ni kituo cha Tuangoma, Mbagala, Mbweni, Mwasonga na Sinza.

Mwakilishi huyo wa Rais, aliwatembelea na kuwajulia hali watoto walioko kituo cha Msimbazi. Baadhi ya vitu vilivyokabidhiwa ni pamoja na pempasi (pampas) za watoto, unga, sabuni, sukari, maziwa na mafuta.

HABARI KITAIFA

# Mchechu asema NHC imeibua ‘wazimu’ uendelezaji wa miradi

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Nehemiah Mchechu, amesema hivi sasa shirika limejizatiti kuibua miradi mingi ya ujenzi wa nyumba ili kuwapatia Watanzania wengi fursa ya makazi na biashara.

Mchechu aliyasema hayo jana wakati wa utiaji saini mkataba wa upangishaji wa hoteli iliyoko katika majengo ya Morocco Square, Kinondoni, Dar es Salaam kati ya NHC na mwekezaji kutoka kampuni ya KingJada Hotels and Apartments.

“Ukiacha mradi huu wa Morocco, tunaendelea na miradi mingi. Ingekuwa ni vichaa, ningesema tumepata wazimu wa kutaka kuibua na kujenga zaidi na zaidi na huo wazimu ni wazimu mzuri sana,” alisema.

Mkurugenzi Mkuu aliishukuru serikali kwa kuliunga mkono shirika na sekta ya miliki nchini kuhimiza uwekezaji ambao umekaribisha wawekezaji wengi nchini kwa ajili ya kuwekeza na kulipatia taifa mapato zaidi.

Mchechu alisema kuwa fursa zinazotolewa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika sekta ya uwekezaji, imechangia kwa kiasi kikubwa kuwasukuma KingJada Hotels and Apartments kuwekeza katika mradi wa Morocco Square.

“Uwapo wa mwekezaji huyu mpangaji katika mradi wetu wa Morocco Square unatokana na mazingira mazuri yaliyowekwa na serikali katika sekta ya miliki. NHC kupitia mradi huu, imetoa fursa pia ya kukuza uchumi wa nchi kupitia mwekezaji huyu na wale wote watakaotoa huduma mbalimbali za kijamii katika mradi wetu,” alisema Mchechu.

Utekelezaji wa mradi wa Morocco Square, mbali na uwepo wa hoteli, pia alisema kuna maduka makubwa ya biashara na nyumba za makazi na kwamba kwa sasa zimebakia shughuli chache ili kukamilisha mradi ambao utaleta chachu kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam.

Mchechu aliipongeza kampuni ya KingJada kwa kuchangamkia fursa ya uwekezaji kwenye hoteli hiyo kwa kuwa watafanya biashara nzuri kwa kuwa eneo la Morocco liko sehemu nzuri ya kufikika kwa urahisi kwa wakazi wa Dar es Salaam. Pia alisema uwapo wa hoteli hiyo utakuwa chachu ya ukuaji wa biashara zingine katika jengo la Morocco Sqaure.

Amesisitiza kuwa NHC imejenga jengo lakini dhamira yake inatimia pale majengo yanayojengwa yatakapopata wanunuzi na wawekezaji, hivyo upatikanaji wa wawekezaji umesaidia shirika kutimiza azma yake ya kuchangia katika kuboresha uchumi wa nchi na kuleta maendeleo nchini.

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa KingJada Hotels and Apartments, Risasi Mwaulanga, alisema wana imani kubwa na NHC kwamba itafika mbali kimalengo na kimkakati hali ambayo itasaidia wawekezaji kufikia malengo yao ya kibiashara.

“Uzoefu wa kampuni yetu katika tasnia ya hoteli nchini India pamoja na uendeshaji wa hoteli za nyota tano ndani na nje ya nchi, tunaamini ubia huu utaleta tija kubwa kwa shirika na mafanikio ya Hoteli ya KingJada yatakuwa chachu ya ukuaji wa biashara zingine katika jengo la Morroco Square,” alisema Mwaulanga.

Aliongeza kuwa kampuni ya KingJada ina uwekezaji mkubwa katika nchi mbalimbali duniani na kuwapo kwake katika jengo la Morocco kutatoa fursa ya ajira na huduma za kihoteli Tanzania.

Katika mradi wa Morocco, kuna majengo manne yakiwamo ya hoteli, jengo la ofisi, jengo la nyumba kwa ajili ya makazi na maeneo ya biashara.

Katika jengo la ofisi zitakuwapo ofisi za Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE) ambalo ni kichocheo kikubwa cha uwekezaji na ukuaji wa mitaji kwa ajili ya maendeleo.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (kulia), akibadilishana hati na Mkurugenzi wa Kampuni ya Mafuta ya Taifa la Falme za Kiarabu (ENOC Group), Saif Al Falas, baada ya kutiliana saini makubaliano ya uwekezaji wa mafuta hapa nchini jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Waziri wa Nishati, January Makamba. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Fisi wa ajabu ang’ang’ania zizini

**Elizabert Seleman,**
SENGEREMA

KATIKA hali isiyokuwa ya kawaida, fisi anayedaiwa wa ajabu amekang’ang’ania kwenye zizi la mifugo na kuzua taharuki kwa wakazi wa Kitongoji cha Mwamatome kijijini Nyakato, Kata ya Tabaruka wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Wakizungumzia tukio hilo, baadhi ya wakazi wa kitongoji hicho waliiambia Nipashe jana kuwa wameshangazwa na fisi huyo kukatalia ndani ya zizi hilo licha ya kufukuzwa na wananchi huku wakilihusisha tukio hilo na imani za kishirikina.

Baadhi ya wananchi hao walisema hawajawahi kuona fisi akiingia kwenye zizi la mifugo na akaacha kuijeruhi mifugo badala yake akalala na kushindwa kufanya chochote zizini humo.

Walidai hawajawahi kuona fisi mkubwa kiasi hicho, wakieleza kuwa walipopiga kelele, fisi huyo hakukimbia, bali alibaki amelala zizini.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyakato, Thomas Sokola, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema kuwa lilitokea usiku wa kuamkia juzi majira ya saa 10 alfajiri alipopigiwa simu na mkuu wa kaya hiyo.

William Sagija, mmiliki wa mifugo hiyo, alidai alisikia kelele usiku na kuamua kwenda nje ili kuangalia kilichokuwa kinatokea.

“Baada ya kumulika, fisi mmoja alikimbia huku mwingine akibaki zizini akiwa amelala, ndipo nilipoamua kupiga kelele kuomba msaada zaidi kwa majirani,” alisimulia.

Kufuatia tukio hilo, Diwani wa Tabaruka, Sospiter Busumabu, aliiomba serikali kuingilia kati suala hilo ikiwamo kutoa kibali ili kuwasaka wanyama.

Jeshi la Polisi wilayani Sengerema lilifika eneo la tukio na kufanikiwa kumuua fisi huyo kwa kumpiga risasi kisha kukabidhi mwili wake kwa Idara ya Maliasili.

# Serikali yatangazia kiama matapeli kuhusu vyeti feki

**Na James Mwanamyoto,**
DODOMA

SERIKALI inawafuatilia ili kuwachukulia hatua matapeli wanaosambaza taarifa za uongo kuhusu kuwarejesha katika utumishi wa umma watumishi waliobainika kughushi vyeti na kuondolewa katika Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alisema hayo jana baada ya kuibuka kwa matapeli wanaoendelea kusambaza taarifa za uongo zikiainisha kuwa serikali imefanya uamuzi wa kuwarejesha watumishi waliondolewa kazini kwa kosa la kughushi vyeti.

Mhagama alisema mara kadhaa ofisi yake imekuwa ikikanusha taarifa ya uongo inayotolewa na matapeli kwa maslahi yao binafsi, ambayo imekuwa ikibadilishwa tarehe mara kwa mara lakini maudhui ni yale yale.

Alisema taarifa hiyo ya uongo ambayo imekuwa ikisambazwa kupitia mitandao ya kijamii, imezua taharuki miongoni mwa jamii, imetengeneza mianya ya rushwa kwa wahusika na imesababisha wahusika kutapeliwa kwa madai ya kusaidiwa kurejeshwa katika utumishi wa umma. Pia alisema taarifa hiyo imewaletea usumbufu wahusika na kuwagharimu kusafiri kwa lengo la kukamilisha mchakato wa kurejeshwa katika utumishi wa umma.

Kutokana na usumbufu huo, Mhagama aliwaonya matapeli wanaoendelea kuupotosha umma kuacha mara moja kitendo hicho ha kuongeza kuwa watakaoendelea kukiuka, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Aidha, Waziri Mhagama ametoa pole kwa wote waliopata usumbufu kutokana na taarifa hiyo ya uongo na kuwataka kuwa makini dhidi ya matapeli hao.

Mhagama amewataka watumishi wa umma na wadau wa utumishi wa umma kuzingatia njia sahihi za kupata taarifa za kiutumishi ambazo zimekuwa zikitumiwa na waajiri kuwafikishia taarifa.

# Ma-DC wapya, waliobaki wafundwa kuhusu mienendo, wajibu kiutendaji

**Na Romana Mallya**

WADAU wamewataka wakuu wa wilaya walioteuliwa kufuata sheria bila kuonea mtu ili watakapoondoka historia iwakumbuke.

Jumatano wiki hii, Rais Samia Suluhu Hassan, aliteua wakuu wa wilaya wapya 37, akiwahamisha vituo vya kazi 48 na wengine 55 wakibakia kwenye maeneo yao. Kati ya hao, wanawake ni 40 na wanaume 100.

Akitoa maoni baada ya uteuzi huo jana, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alitaka wateule wote wafuate miongozo na sheria bila kuonea watu.

"Wakaitendee haki huduma ya jamii kwa maana kwamba wao ni watumishi wa umma na si watawala. Wakitumikia bila migogoro historia itawakumbuka.

"Wale walioachwa wasione kama wamepewa adhabu, watambue mteuaji anayo nafasi ya kuteua na kutengua na miongoni wamo waandishi wenzetu, tunawakaribisha waje kwenye taaluma tulisukume gurudumu," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA - TAN), James Marenga, aliwataka wateule wapya na wanaoendelea kuhakikisha wanafanya kazi vizuri na vyombo vya habari kama Rais Samia Suluhu Hassan alivyotoa uhuru wa habari.

"Rais ameonyesha nia thabiti ya kuhakikisha kunakuwa na uhuru wa habari.

Hata jitihada zake za kuhakikisha sheria ya habari ikiwamo ya huduma ya habari na zingine zinafanyiwa mabadiliko, ameonyesha utayari wa kufanya kazi na waandishi wa habari.

"Kwa hiyo wakuu wa wilaya walioteuliwa na wanaoendelea wahakikishe wanawapatia waandishi wa habari taarifa kama zinavyotakiwa bila kuficha ukweli kwenye maeneo yao," alisema.

Pia alisema suala la kukamata waandishi wa habari na kuwekwa ndani kwa kutumia mamlaka yao, wafahamu kuwa uhuru umetolewa hivyo wasiingie katika mkondo wa kudumaza tasnia hiyo kwenye maeneo yao.

Mchambuzi wa Siasa, Nassoro Katunda ambaye ni Mhadhiri Msaidizi Idara ya Sosholojia na Anthropolojia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alisema utamaduni wa kuteua umekuwa wa siku nyingi.

"Huenda mabadiliko hayo yaliyofanywa na Rais ya kupanga safu yanalenga na kuona kwamba wale hawakufanya vizuri wanaondolewa na kuwaweka wale wanaweza kumsaidia Mheshimiwa Rais katika uboreshaji wa utendaji kazi.

"Wako waliohamishwa kutoka eneo moja kwenda lingine kwenda kusaidia kazi maeneo mengine.

Kwa maoni yangu ninafikiri nafasi hizi ziwe zinapimwa na mwelekeo wa nchi nini inataka, ndiyo maana muda mwingine tunaona isiwe tu watu wachaguliwe wa chama kinachoshikilia dola, inapaswa iwe mchanganyiko, kwa kuangalia mtu mwenye uwezo wa kusaidia Watanzania," alishauri.

Pia alishauri katika nafasi za uteuzi watu badala ya kuteuliwa, wawe wanachaguliwa kwa sababu wakati mwingine mtu hupelekwa eneo ambalo wananchi hawamjui, hivyo dhana ya kupeleka maendeleo kwa wananchi inakuwa na changamoto.




Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Kilombero Sugar Company Ltd, Ephraim Mafuru, akizungumza katika kikao kazi na taasisi mbalimbali za fedha kilichoandaliwa na Taasisi ya Financial Sector Deepening Trust (FSDT), jijini Dar es Salaam hivi karibuni, kilicholenga kuweka mikakati ya kusaidia wakulima wa miwa wa Bonde la Kilombero. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## AG akabidhiwa 'kilio' cha waandishi habari

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) inapitia mapendekezo ya maboresho ya Sheria ya Huduma za Habari (2016) baada ya kukabidhiwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Hatua hiyo inafanyika kabla ya ofisi ya AG kuwasilishwa bungeni muswada wa marekebisho ya sheria hiyo ili kusomwa.

Waziri wa Habari, Nape Nnauye amethibitisha kuwa maoni na mapendekezo ya wadau mpaka sasa yamekabidhiwa kwenye ofisi wa AG kama inavyoelekezwa kwa mujibu wa taratibu.

"Kuhusu mchakato wa mapitio ya Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya Mwaka 2016, ninafurahi kuwajulisha kuwa baada ya majadiliano ya muda mrefu na wadau mbalimbali, hatimaye majadiliano yamekamilika na nyaraka za maeneo yote tuliyokubaliana kufanyia mabadiliko zimewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu," alisema Nape akiwa jijini Dodoma juzi alipozungumzia hatua zilizofikiwa kuhusu mchakato wa mabadiliko sheria hiyo.

Deodatus Balile, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), alisema mchakato huo mpaka kufikishwa bungeni una hatua zake na kwamba kinachofanywa na serikali ni utaratibu wa kawaida katika kuelekea mabadiliko ya sheria hiyo.

"Mchakato bado upo kwenye mstari uleule, mpaka sasa matumaini yetu yapo juu katika kufikia kile tunachokihitaji. Serikali bado inapitia mapendekezo yetu katika hatua zilezile za kawaida.

"Sisi tungetamani kasi zaidi kama alivyoshauri Mheshimiwa Rais Samia (Suluhu Hassan) kwamba tulimalize," alisema Balile akizungumzia kauli hiyo ya Nape kwamba mapendekezo ya wadau wa habari yako kwenye Ofisi ya AG.

Muungano wa wadau wa habari (CoRI) tayari umeshafanya vikao viwili na serikali kuelekea mabadiliko ya sheria hiyo iliyoibua ukosoaji tangu kutungwa kwake takribani miaka saba iliyopita.

Wadau hao nchini wanashauri marekebisho kwenye vipengele mbalimbali vya sheria hiyo ikiwa ni pamoja na kifungu cha sita (e) kinachoeleza magazeti kupatiwa leseni kila mwaka badala ya usajili wa moja kwa moja.

Pia marekebisho dhidi ya kifungu cha saba (2)(b)(iv) kinachoelekeza vyombo vya habari kutangaza au kuchapisha habari na masuala yenye umuhimu kwa Taifa kadri itakavyoelekezwa na serikali, wadau wakielezea kuwa kipengele hiki kinaingilia uhuru wa uhariri.

# India yajivunia miradi ya ujenzi wa viwanda

**Na Romana Mallya**

SERIKALI ya India imesema uhusiano wa kibiashara kati yake na Tanzania unatarajiwa kukua zaidi mwaka huu kutokana na uwekezaji uliofanywa na unaoendelea kufanywa na kampuni zake nchini, ukiwamo ujenzi wa kiwanda cha sukari kinachojengwa jijini Dodoma.

Jijini Dar es Salaam jana, Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan, alibainisha matarajio yao hayo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu uhusiano ulivyokua kati ya nchi hizo ndani ya mwaka mmoja.

Balozi huyo alieleza namna nchi hizo mbili zilivyonufaika kupitia uhusiano huo na kuwezesha kukua kwa biashara, uwekezaji na kuvutia wawekezaji wa India kuja Tanzania kuwekeza.

"Kwa sasa tunafurahi uhusiano wa kibiashara unakua kwenye nchi hizi, tumeona wawekezaji kutoka India wanawekeza Tanzania na tayari wameshafungua viwanda mkoani Dodoma ambako wanajenga kiwanda kikubwa cha kisasa cha kuzalisha sukari kitakachokamilika mwezi Desemba mwaka huu na kiwanda kingine cha kuzalisha chanjo za wanyama kitakachojengwa nje ya Dar es Salaam," alisema.

Alisema katika kipindi cha mwaka jana, kampuni mbalimbali za India ziliwekeza kwenye sekta mbalimbali nchini, zikiwamo afya, elimu, kilimo na madini.

Alisema uhusiano na ushirikiano baina ya nchi hizo unatarajiwa kuongezeka mwaka huu baada ya baadhi ya kampuni za India kuja kuwekeza kwenye maeneo mbalimbali.

Alisema kuwa kwa mwaka jana, wawakilishi wa kampuni mbalimbali za India walitua nchini kwa lengo la kutafuta fursa za uwekezaji na nyingine kushiriki maonyesho ya bidhaa mbalimbali wanazozalisha.

Alisema wanatarajia hadi kufika mwezi Machi au Aprili mwaka huu, biashara kati ya nchi hizo mbili itafikia dola za Marekani bilioni sita.

Alisema wanatarajia kuzungumza na Serikali ya Tanzania ili wafanyabiashara kati ya nchi hizo walipe kwa kutumia fedha inayotumika kwenye nchi husika.

Kadhalika, Balozi huyo alisema kuwa kwa mwaka huu, India itahamasisha wawekezaji katika Sekta ya Fedha kutoka Tanzania kwenda kuwekeza India kwa kufungua benki.

Balozi huyo pia alisema kwa mwaka huu wataendelea kupeleka India kupata mafunzo makundi mbalimbali ya Watanzania kutoka sekta tofauti.

Pia alisema wanatarajia kujenga maeneo maalum ya uwekezaji nchini na kwa sasa wako katika mazungumzo na serikali.

Alisema biashara ya usafirishaji maparachichi ya Tanzania kwenda India imekua kutokana na nchi yao kuondoa ushuru wa forodha.

Akizungumzia ushirikiano wa kisiasa, Balozi Pradhan alisema utaendelea kuimarika, akikumbusha kuwa mwaka jana mawaziri kutoka sekta tofauti walizuru India kikazi na kubadilishana uzoefu na wenyeji wao.



Mhandisi John Mshwerwa kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET), akipanda mti katika Shule ya Msingi Mapambano Mikocheni B, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni jitihada za baraza hilo kuunga mkono kampeni ya utunzaji mazingira. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Adaiwa kubambwa na dhahabu kilo 17.7

**Na Samson Chacha,** TARIME

JESHI la Polisi Mkoa wa Kipolisi wa Tarime Rorya, katika kipindi cha Desemba hadi Januari 26, mwaka huu, kupitia msako unaoendelea, limemkamata mkazi wa kitongoji cha Makaranga Nyamongo (jina limehifadhiwa) akiwa na mfuko wenye mawe ya dhahabu yenye uzito wa kilogramu 17.68.

Sambamba na madini hayo, jeshi hilo pia limekamata meno manne ya tembo, magunia 35 ya mirungi ndani ya gari lenye namba ya usajili T 343 DWE, pikipiki yenye namba MC 242 DDE iliyokuwa na meno ya tembo na kufyeka ekari moja ya bangi.

Kamanda wa Mkoa wa Kipolisi wa Tarime Rorya, Kamishna Msaidizi (ACP) Geofrey Sarakikya, alisema pia jeshi limewakamata watu kadhaa wanaotuhumiwa kuhusika na uhalifu huo huku msako zaidi ukiendelea.

"Katika msako unaoendelea wa wahalifu, tumefanikiwa kuwakamata watu kadhaa.

Januari 11 tulimkamata mkazi wa kitongoji cha Makaranga Nyamongo (jina linahifadhiwa kwa sababu wenzake bado wanasakwa) akiwa na kilogramu 17.68 za mawe ya

dhahabu ndani ya mgodi wa Barrick North Mara. Mtuhumiwa huyo alikuwa na wenzake wawili ambao walifanikiwa kutoroka na tunawasaka," alisema.

Kamanda Sarakikya alisema Januari 18, askari wa Kituo cha Sirari mpakani waliokuwa doria, walimwona mtuhumiwa akiwa na begi akivuka mpaka kuingia nchini Kenya na walipojaribu kumfuatilia kwa nyuma, alitupa begi hilo na kutorokea Isebania nchini Kenya.

Alisema baada ya kulichukua, walilipekua na kukuta ndani kuna vipande viwili vya meno ya tembo vyenye uzito wa kilogram 3.5 na juhudi za kumsaka mtuhumiwa aliyetoroka zinaendelea.

Sarakikya alitaja matukio mengine na kukamatwa kwa vitu vikiwamo mirungi magunia 35 yenye uzito wa kilogramu 524 yaliyokuwa yamepakiwa ndani ya gari aina ya Toyota Probox lenye namba za usajili T 343 DWE. Alisema magunia hayo yalifaulishwa Kitongoji cha Nyangiri Kijiji cha Kogaja kutoka gari la Kenya lenye namba za usajili KDD 419 Y aina ya Toyota Wish lililokuwa likiendeshwa na dereva Mmeru kutoka nchini Kenya huku dereva wa gari la Probox la Tanzania akitoroka na juhudi za kumtafuta zinaendelea.

Katika hatua nyingine, alisema Jeshi la Polisi lilimkamata mkazi wa Kitongoji cha Nyamilama Kijiji cha Masanga akiwa na vipande viwili vya meno ya tembo akiwa amepakia kwenye pikipiki yenye namba za usajili MC 242 DDE yenye uzito wa kilogramu 35.84.

Aidha, alisema Januari 13, mwaka huu, katika Kijiji cha Nyamasana, Wilaya ya Rorya, walikamatwa watu wanne waliolima shamba ekari moja ya bhangi.

Licha ya kukamatwa kwa watu hao, alisema polisi walifyeka shamba hilo na kuwahoji watuhumiwa ili kupata mtandao wa wanaolima, kuuza na wanaonunua bhangi ili hatua kali zichukuliwe dhidi ya mtandao huo.

# NBC yatoa zawadi kwa washindi kampeni yake

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imetoa zawadi mbalimbali zikiwamo baiskeli, pikipiki na trekta kwa washindi wa mpango wa pili wa kampeni ya benki hiyo ijulikanayo 'Vuna Zaidi na NBC Shambani' inayohusisha Mkoa wa Mtwara.

Kampeni hiyo inalenga kuchochea kiwango cha uzalishaji wa zao la korosho na mazao mengine mkoani humo.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya kuhitimisha kampeni hiyo sambamba na kukabidhi zawadi kwa washindi ikiwamo kukabidhi trekta kwa Chama Kikuu cha Ushirika cha Masasi, Mtwara (MAMCU), Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas, alisema zawadi hizo zimekuja wakati mwafaka wakati mkoa ukitekeleza mkakati wa kuongeza uzalishaji wa korosho.

Alisema mkoa unatekeleza mkakati wa kuongeza uzalishaji kutoka tani 400,000 za sasa hadi tani 700,000 ifikapo mwaka 2025.

"Ni mpango wa serikali kuona sekta ya kilimo inakua kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030, tunashukuru kuona benki ya NBC inashiriki kikamilifu katika kufanikisha azma hiyo kupitia NBC 'Vuna Zaidi na NBC Shambani'" alisema Kanali Abbas.

Kiongozi huyo aliwaomba wataalamu wa kilimo mkoani humo kuwatembelea wakulima mara kwa mara ili kuwapa elimu itakayowawezesha kuzalisha korosho bora.

Pia aliwataka wakulima kuhakikisha wanahifadhi fedha zao benki pamoja na kuwa na nidhamu nazo ili kuwekeza zaidi kwenye ununuzi wa vifaa vya kilimo cha kisasa na uzalishaji na kujikwamua kiuchumi.

Mkurugenzi wa Fedha wa NBC, Waziri Barnabas, alisema tangu kuanza kwa kampeni hiyo, jumla ya washindi 73 wakiwamo mkulima mmoja mmoja, vyama vya msingi (AMCOS) na vyama vikuu vya ushirika kutoka mkoa huo waliibuka washindi na kupata zawadi mbalimbali likiwamo trekta, maguta mawili na pikipiki 12.

Pia kupitia kampeni hiyo iliyoanza Oktoba 13, mwaka jana, walitoa pampu za kupulizia dawa miti ya mikorosho 40, baiskeli 20 vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 150.

"Bado ninatoa wito kwa wakulima kuendelea kupitisha fedha zao za malipo ya korosho kupitia akaunti zao za 'NBC Shambani' ili kupata fursa ya kufurahia zaidi manufaa yatokanayo na akaunti hiyo," alisema.

Alisema benki hiyo imedhamiria kushirikiana na wakulima ili kuhakikisha wanaboresha sekta ya kilimo na kwamba mbali na kampeni hiyo, benki imekuwa ikitoa mikopo mbalimbali kwa vyama vya msingi katika mikoa hiyo ili kusaidia utendaji kazi wao katika shughuli zinazohusiana na uzalishaji wa korosho.

Washindi wa droo hiyo waliishukuru NBC kwa kuandaa kampeni hiyo ambapo walieleza kuwa imekuwa msaada mkubwa.

"Tunashukuru sana Benki ya NBC kwa zawadi ya trekta hili kwa kuwa itatusaidia sana kufikia malengo yetu,

"Pia tunaahidi kuendelea kuelekeza fedha zetu kupitia akaunti ya 'NBC Shambani' ili kujishindia zawadi nyingi zaidi," alisema Siraji Mtenguka, Mwenyekiti wa MAMCU ambaye taasisi yake imejishindia zawadi ya trekta kupitia kampeni hiyo kwa mara ya pili mfululizo.

# Mkurugenzi ataka fursa ajira kikanda zitumiwe

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Huduma za Ajira Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Joseph Nganga, amezishauri nchi za ukanda wa Mashariki na Pembe ya Afrika kuongeza ushirikiano ili raia wa nchi hizo wanufaike na fursa za ajira zinazojitokeza.

Akizungumza kwa niaba ya Serikali ya Tanzania kwenye mkutano wa kanda hiyo uliofanyika Zanzibar wiki hii, Nganga alisema ushirikiano wa nchi hizo utaongeza ufanisi katika kuwezesha ajira za staha kwa raia wake.

"Ninashauri nchi hizi kuweka utaratibu wa kujadili na kuingia makubaliano na nchi zenye fursa za ajira kama ukanda, kutekeleza programu za kuwajengea ujuzi stahiki raia wanaokwenda kufanya kazi nje ya ukanda.


"Pia kuweka mifumo ya kielektroniki kuratibu michakato ya uhamaji nguvukazi pamoja na kukusanya, kuchambua takwimu na kutoa taarifa za uhamaji nguvukazi," alisema.

Kiongozi huyo alisema uhamaji nguvukazi ni jambo linaloendelea kukua kutokana na kupanuka kwa ushirikiano wa kikanda pamoja na maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Alisema uhamaji wa nguvukazi una mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi husika kwa kuongeza fursa za ajira na hivyo kukuza uchumi wa nchi husika.

Mkutano huo ulishirikisha nchi za Kenya, Tanzania, Somalia, Ethiopia, Uganda, Djibouti, Sudan Kusini na Sudan, ukilenga kubadilishana uzoefu na kuweka mikakati ya pamoja kuhusu masuala ya uhamaji nguvukazi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII




# Bodi ya Ligi, TFF, mechi za usiku zinaziumiza klabu

**SASA** imekuwa kawaida kwa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na zile za Kombe la FA kuchezwa usiku katika viwanja vyenye uwezo wa kufanya hivyo.

Mara nyingi mechi za timu huanza kuchezwa kati ya saa 1:00 usiku na 3:00 usiku na sababu kubwa inatajwa kwamba, kuwapa nafasi mashabiki wanaotoka kazini kwenda kutazama mechi hizo uwanjani.

Lakini kinyume chake ni kwamba, sasa mashabiki wamekuwa wakijazana hotelini, baa, sehemu zingine za starehe, majumbani mwao na hata kwenye vibanda vya kuonyesha michezo maarufu 'vibanda umiza' ili kufuatilia mechi hizo.

Kuna wakati Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ilisema kuwa iko katika mchakato wa kupata mshauri wa kufanya tathmini kugungua kwa nini idadi ya watu wanaohudhuria mechi uwanjani inashuka, hivyo kusababisha mapato ya mlangoni kupungua.

Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, alinukuliwa akisema idadi ya mashabiki uwanjani imepungua na bodi ipo katika kufanya tathmini na kutafuta ufumbuzi wa sababu ya watu kutoingia uwanjani kama ilivyo miaka ya nyuma.

Alisema wapo kwenye kipindi cha mpito, hivyo wanatakiwa kutafakari na kuangalia jinsi ya kupunguza viingilio. Ingawa ukweli ni kwamba sio viingilio, bali ni muda wa mechi hizo.

Mashabiki wa mikoani huwa wanajazana viwanjani na hasa zinapokwenda klabu kubwa mbili maarufu na kongwe nchini Simba na Yanga.

Mashabiki wanaotajwa kuwa wamepungua viwanjani si wa Singida Big Stars, wala Coastal Union, ni wa Simba na Yanga tu. Huu ndiyo utamaduni wa soka la Tanzania tangu enzi na enzi.

Sasa tukiangalia ukweli kwanini mashabiki wengi hawaendi viwanjani, sababu kubwa ni muda wa mechi zinazochezwa hasa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa ambapo huanza saa 1:00 usiku. Hii ni moja ya sababu kubwa kupungua kwa mashabiki viwanjani.

Kwa sasa Jiji la Dar es Salaam limekuwa kubwa, kuna wakazi wa Goba, Mbezi Louis, Mbezi Beach, Bunju, Boko, Kisemvule, Chanika na sehemu nyingine nyingi zilizo nje ya jiji.

Kuna mashabiki wengine wanatoka Bagamoyo mkoani Pwani hadi Chalinze kuangalia mechi. Hawa ukiwawekea mechi ya saa moja usiku tatizo lao inakuwa ni usafiri wakati wa kurejea makwao.

Kutoka kwa Mkapa usiku wa saa tatu, hadi kufika makwao ni usiku wa manane kutokana na umbali pamoja na shida ya usafiri. Atapanda usafiri wa umma maarufu kama daladala ambapo bei imeongezwa mara mbili ya kawaida, akishuka anapokwenda anaweza kupanda tena daladala nyingine ya kuingia kwenye viunga vya ndani.

Halafu pia atashuka na kupanda bodaboda ili kumfikisha nyumbani kabisa. Gharama za usafiri usiku mara nyingi inakuwa kubwa. Halafu muda atakaolala kesho yake anatakiwa aamke alfajiri kwenda kibaruani. Shabiki huyo ni lazima aamue kubaki mitaa yake ya nyumbani na kuangalia kwenye kibanda umiza.

Cha kushangaza wakati Bodi kwa sasa inaonekana kupenda sana mechi za usiku, Ulaya hasa kwenye Ligi za England wameonekana kupunguza sana mechi za usiku mnene.

Hispania nao wamefanikiwa sana, kwa sasa hata Watanzania wamekuwa wakishuhudia Barcelona na Real Madrid zikicheza hata saa mbili za usiku, tofauti na zamani mechi zao zinakuwa usiku mnene kuanzia saa nne, tano hadi sita.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mpira wa pasi nyingi bila faida umepitwa na wakati

**KWA** muda mrefu ambao nimefuatilia soka la Tanzania pamoja na mashabiki wake, nilichogundua ni kwamba Wabongo wanapenda sana soka la 'shule' na maonyesho zaidi, badala ya matokeo.

Ndiyo maana mchezaji akija hapa nchini akiwa hapendi kupiga chenga, kanzu, matobo na kurudisha mpira nyuma, wanamhesabia kama ni mchezaji wa kawaida tu.

Wabongo wanapenda zaidi wachezaji wanaocheza na jukwaa, ila tu atasemwa na kusakamwa kama timu haipati ushindi. Ikipata wewe ndiyo staa.

Mchezaji yoyote anayekuja nchi na kucheza soka la moja kwa moja kwa ajili ya kuipatia matokeo anachukua muda mrefu kueleweka.

Hii imewafanya hata wachezaji wengi kutoka nje, hata kama alikuwa anacheza aina fulani ya soka la kasi, la moja kwa moja kwa ajili ya kuisaidia timu, ili kukubalika na mashabiki wamekuwa wakibadilika na kucheza soka ambalo linapendwa.

Ni soka lisilotumia sana nguvu, halina kasi, kupasiana wakati wamejikusanya kwa pamoja kama wapo mazoezini na hata wakifika karibuni na goli, basi huoni kasi ya kusaka bao, badala yake unaweza kuona mpira unarudishwa nyuma.

Wenyewe wanasema wanaiga soka la Ulaya, lakini ukiangalia zaidi utakuwa si kweli, huko kuna soka la kasi sana na hawanyati kama wachezaji wa hapa wanavyofanya.

Wiki hii nimewasikia watu wawili wakisema mambo ambayo hata mimi yalikuwa wananishangaza kuhusu soka letu na hasa kwenye klabu zile kubwa.

Nimemsikia Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira, akisema falsafa yake ni kucheza soka la kushambulia zaidi.

Na kweli, ukiangalia kwa vitendo, mechi mbili tu ambazo Simba ilicheza dhidi ya Mbeya City, ikashinda mabao 3-2 na ile dhidi ya Dodoma Jiji utaona kwa kiasi fulani kuna kitu anakiingiza ndani ya kikosi.

Ndiyo maana baadhi ya mashabiki wa Simba wanalalamika kuwa hawajaona aina yake ya soka ambalo wamezoea. Ile ya pasi nyingi na kwenda kumshambulia mpinzani taratibu.

Kwa sasa wachezaji wa Simba hawana 'doji' nyingi, wanakwenda kushambulia kwa kasi na kurudi kukaba kama mbwa mwitu.

Nina uhakika, iwapo wachezaji wa Simba watazoea mfumo huu inaweza kuwa timu hatari zaidi kama yeye mwenyewe Robertinho anavyosema kuwa anataka kutengeneza timu tishio.

Ni kiasi tu cha wanachama na mashabiki wa Simba wampa muda.

Baada ya mechi dhidi ya Ruvu Shooting na Yanga kushinda bao 1-0, mmoja wa viongozi wa zamani wa soka nchini na klabu ya Simba, Ismail Aden Rage naye alionyesha kushangazwa na timu nyingi za Ligi Kuu kucheza mpira wa maonyesho wa pasi nyingi zaidi kuliko kutafuta mabao.

"Wamejitafutia wenyewe, wala Yanga isingeshinda bao moja, wametumia muda mwingi kuuchezea mpira badala ya kushambulia moja kwa moja.

Kama wangeshambulia moja kwa moja nadhani wangepata na hiyo nimeona ni udhaifu wa timu nyingi kwa sasa hapa Tanzania, wamekuwa wakiiga mpira wa kupasiana sana mpira kwa pasi ambazo hazina sababu za msingi badala ya kufanya mashambulizi, ili wapate pointi nyingi kwenye kuumiliki mpira. Utaona timu inakwenda mbele halafu ghafla utaona wanarudisha tena mpira nyuma, sasa huo siyo mpango mzuri hata kidogo kama timu inataka ushindi." Yalikuwa ni maneno ya Rage.

Hapa unapata tafsiri kuwa kuna aina ya soka ambalo Bongo linachezwa hata wazungu wenyewe hawachezi. Wao wanapasiana kwa ajili ya kuwafungua wapinzani na kutafuta nafasi, wala si kufurahisha jukwaa. Halafu wanacheza kwa kasi na kukimbia, si kutembea.

Kwa maneno haya ya Robertinho na Rage, inabidi sasa klabu zetu zibadilike, hasa wanachama na mashabiki wake ambao ndiyo wanawatia 'ujinga' wachezaji wao, badala ya kusaka ushindi kwa ajili ya timu, wanafurahisha jukwaa na kusaka sifa binafsi.

# Watu 139 wafa migodini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TUME ya Madini imewataka wachimbaji wadogo wa madini kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo ili kuepusha ajali zinazotokea migodini ambazo katika kipindi cha miaka miwili zimesababisha vifo vya watu 139 na majeruhi 59.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, Yahaya Samamba, aliyasema hayo jana kupitia hotuba yake iliyosomwa na Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka tume hiyo, Dk. Anird Gesase, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku mbili ya wachimbaji wadogo wa madini Kanda ya Kati yanayofanyika mjini Singida.

Samamba alisema katika kipindi cha kuanzia 2018/2019 hadi 2019/2020 kuliripotiwa matukio 99 ya ajali migodini yaliyosababisha vifo vya watu 139 na majeruhi 59, hali ambayo si afya kwenye sekta ya madini.

Alisema uchunguzi uliofanywa umeonyesha kuwa ajali hizo zinasababishwa na kuanguka kwa mashimo ya uchimbaji na kukosekana kwa hewa ndani ya mashimo ya uchimbaji.

Alisema pia utafiti unaonyesha ajali nyingi zinatokea migodini kutokana na kutozingatia masuala ya usalama, afya na utunzaji mazingira miongoni mwa wachimbaji.

"Shughuli za uchimbaji na uchenjuaji madini zina manufaa mbalimbali kwa wachimbaji, wananchi na taifa kupitia fursa ya ajira, biashara na tozo, lakini shughuli hizo huambatana na matukio ya ajali na madhara ya kiafya na uharibifu wa mazingira," alisema.

Aliongeza kuwa wachimbaji lazima wazingatie sheria kuhusu baruti ya mwaka 1963 na kanuni zake za mwaka 1964 ili kukabiliana na masuala ya usalama, afya na utunzaji wa mazingira migodini.

Baadhi ya wachimbaji wadogo walilalamikia gharama za kibali cha kulipia baruti ambazo wanatozwa Sh. 100,000 huku kibali hicho kikidumu kwa mwezi mmoja na hivyo kuiomba serikali kuondoa tozo hizo.

Wachimbaji wadogo wa madini wanapewa mafunzo hayo ili kuhakikisha shughuli za uchimbaji na uchenjuaji madini zinafanyika kwa kuzingatia usalama, afya na utunzaji mazingira.



Mafundi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (DAWASA), wakiweka mabomba kwenye mradi wa Mbopo Chekanao, Kata ya Mabwepande, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TBS yamulika ubora kwa waagizaji nondo, mabati

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limewataka wazalishaji na waagizaji wa bidhaa za nondo, mabati na bomba kuzingatia viwango vya ubora ili kuondoa malalamiko ya watumiaji wa bidhaa hizo.

Kaimu Mkurugenzi wa Utekelezaji wa Sheria wa TBS, Candida Shirima, alitoa angalizo hilo jana wakati wa mkutano na waagizaji, wasambazaji na wazalishaji wa bidhaa hizo.

"Iwapo mtumiaji atanunua bidhaa zisizokidhi viwango mnasababisha malalamiko ya bidhaa zenu na thamani ya fedha inakuwa haipo kwa hiyo kila mmoja wenu anawajibika kuhakikisha anazingatia matakwa ya ubora," aliagiza.

Alisema waagizaji na wazalishaji wa bidhaa hizo wanapaswa kuzingatia ubora ili kuwe na ushindani wa haki kwenye soko, kulinda mazingira na kuwezesha wanunuzi kupata bidhaa zinazoendana na thamani ya fedha.

Alisema ili kuimarisha ubora wa mabati, koili za kutengenezea mabati, nondo na bidhaa zingine za chuma wazalishaji hao wanapaswa kuhakikisha zinakuwa na viwango vya kitaifa na kimataifa.

Alisema kila mzalishaji na mwagizaji wa bidhaa hizo anapaswa kuhakikisha zinaandikwa taarifa zote muhimu ambapo kwa mujibu wa viwango vya kimataifa bidhaa hizo lazima ziandikwe daraja, jina la mzalishaji, vipimo na namba za toleo.

Alisema TBS itaendelea kusimamia kikamilifu jukumu la kuhakikisha ubora wa bidhaa hizo nchini ikiwa ni pamoja na kuzifanyia ukaguzi na uchunguzi wa kimaabara kabla ya kuingia nchini.

Alisema shirika hilo litaendelea pia kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo ili kuhakiki ubora wa bidhaa zinazozalishwa.

"TBS pia inawajibika kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara, kutoa elimu ya ubora kwa wadau na kuwachukulia hatua stahiki wale wote watakaobainika kukiuka matakwa ya sheria," alisema.

Ofisa huyo alisema TBS iliamua kuandaa mkutano huo kwa lengo la kukuza uelewa wadau hao kuhusu matakwa ya Sheria ya Viwango Sura 130 na kanuni mbalimbali za viwango vya kimataifa vya bidhaa hizo.

Alisema kwa kuwa azma ya serikali ni kujenga uchumi imara, endelevu na wenye nguvu na ushindani, lazima bidhaa zinazozalishwa ziwe imara.

## Mitambo kuchakata takatope kujengwa

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa mitambo minane ya kisasa ya kuchakata takatope itakayoleta unafuu wa maisha na kuchangia uboreshaji wa sekta ya afya na makazi jijini Dar es Salaam.

Mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano wa Benki ya Dunia (WB) kupitia mradi wa uboreshaji wa sekta ya maji awamu ya pili ambapo umehusisha ujenzi wa mitambo minane ya kisasa ya kuchakata takatope kwenye wilaya za Kinondoni, Temeke, Kigamboni, Ubungo na Ilala.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, Msimamizi wa Kitengo cha Usafi wa Mradi kutoka Kitengo cha Usafi wa Mazingira DAWASA, Amon Gracephord, alibainisha utekelezaji wa mradi huo umeanza kwenye maeneo ya Mabwepande, Gezaulole, Kimbiji, Kisopwa, Vijibweni, Vikunai, Mtoni na Zingiziwa. "Ujenzi wa mitambo hii unalenga kuongeza ufanisi kwa miundombinu ya majitaka sambamba na yale mabwawa ya Vingunguti na Kurasini pamoja na mitambo ya kuchakata takatope iliyoko Mburahati, Wailes, Mlalakuwa na Toangoma," alisema.

"Tunalenga kupunguza umbali wa maliwato ya mwananchi na eneo ambako yatatupwa uchafu huo, ambao kwa sasa unafanya gharama za huduma ya unyonyaji majitaka kuwa juu. Ila eneo la kuchakata linapokuwa karibu inamaanisha hata gharama za huduma zitapungua," alisema. Gracephord alieleza faida za mradi kuwa ni pamoja na kuzalisha mbolea inayofaa kutumika katika bustani za miti na majani na gesi inayoweza kupikiwa.

"Pamoja na kuchakata takatope, mitambo hii ina uwezo wa kuzalisha mbolea, gesi na maji ya kumwagilia bustani kama ambavyo inafanyika katika mitambo yetu ya Mburahati, Mlalakuwa na Toangoma," alisema.

Alisema mkandarasi wa mradi huo tayari ameshapatikana na ujenzi wa mitambo hiyo unategemewa kuanza mwezi ujao baada ya hatua za awali kukamilika.

Ofisa Afya Wilaya ya Ilala, Reginald Mlay, alisema mradi wa mitambo ya kuchakata takatope una manufaa makubwa katika sekta ya afya kwa kuwa utapunguza hatari ya wananchi kupata magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu.

Mradi wa uboreshaji usafi wa mazingira unahusisha ujenzi wa mitambo minane ya kisasa ya kuchakata takatope yenye uwezo wa kuchakata lita 780,000 kwa siku, ujenzi wa mifumo rahisi 12 ya uondoshaji majitaka majumbani, ujenzi wa vyoo vya umma 30 na utagharimu takribani Sh. bilioni 35 na unatarajiwa kuhudumia wakazi takribani milioni 1.7.

# Viongozi wa SACCOS wadaiwa kutafuna mil. 300/- za walimu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewaagiza viongozi wa serikali wilayani Iramba kuwakamata na kuwaweka ndani waliokuwa viongozi wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Walimu Iramba (CHAMWAI) kutokana na kushindwa kuwalipa walimu fedha zao zaidi ya Sh. milioni 300.

Amesema viongozi hao wakikamatwa, wafikishwe kwenye kikao kitakachofanyika Jumanne ijayo kwenye ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ili kujibu tuhuma zinazowakabili.

Serukamba aliagiza hayo jana alipozungumza na walimu zaidi 100 ambao walifika ofisini kwake kulalamika kutolipwa fedha hizo tangu mwaka 2012.

"DC (Mkuu wa Wilaya) ninataka unitafutie wale viongozi wa zamani wa CHAMWAI kwa kuwakamata uwatie ndani mpaka tutakapokutana ili tuje tukutane nao Jumanne," aliagiza.

Alisema katika kikao hicho pia wawapo maofisa ushirika walioshiriki jambo hilo tangu mwanzo, wakurugenzi wa halmashauri za Iramba na Mkalama, mweka hazina na viongozi wa sasa wa CHAMWAI.

"Ninataka tupate mwelekeo mzuri tangu chama kilipoanzishwa fedha zilizokuwa zinachangwa zilikuwa zinapelekwa wapi na zilivyoanza kutoka zilikuwa zinakwenda wapi," alisema.

Serukamba alisema katika chama hicho kuna matatizo mengi, akitolea mfano katika moja ya nyaraka za kuomba mkopo, alitia saini Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida wakati chama hicho kipo Wilaya ya Iramba.

Mwalimu Nalogwa Temaec, akizungumza kwa niaba ya walimu wenzake, alimweleza Mkuu wa Mkoa kuwa walianza kuchangia Sh. 10,000 kila mwezi ambazo zilikuwa zikikatwa moja kwa moja kwenye mishahara yao na kuingizwa kwenye akaunti za chama.

"Tulikuwa tunaweka fedha zetu na kukopa, wakati tunakopa tulikuwa tunarudisha kwa riba tukiwa na maana baada ya kustaafu kazi, tutalipwa fedha zetu na chama wakati tukisubiri mafao ya serikali," alisema.

Aliongeza kuwa tatizo lilianza kujitokeza baada ya wakurugenzi wa halmashauri kuingia tamaa na kuanza kuchukua mapato ya chama na kuyatumia kwa kazi nyingine.

Kwa mujibu wa ripoti ya ukaguzi iliyofanywa na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Kamati ya Mikopo ya chama hicho haikutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuwa ilitoa mikopo bila kufuata utaratibu.



Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood (kulia), akigawa zawadi ya majaketi yenye viakisi mwanga yapatayo 1,500 kwenye moja ya vituo vya bodaboda, eneo la Hipohipo, Kata ya Mazimbu, Manispaa ya Morogoro jana. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Abood awapa mbinu bodaboda kupatiwa mikopo ya serikali

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood (CCM), amewataka vijana wanaosafirisha abiria kwa kutumia pikipiki, maarufu bodaboda, kuanzisha vikundi na kuvisajili ili wanufaike na mikopo ya fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya maendeleo yao.

Abood alitoa rai juzi alipotembelea maeneo mbalimbali ya vituo vya kazi vya bodaboda na kuwakabidhi zawadi za majaketi yenye viakisi mwanga yapatayo 1,500 yakiwa na ujumbe maalum wa kuhamasisha utalii.

Alisema hatua hiyo ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan katika kuliepusha kundi hilo kubwa na ajali barabarani hususani nyakati za usiku.

Abood alisema madereva wa bodaboda ni kundi kubwa, hivyo wakijiunga kwenye vikundi na kuvisajili, watakuwa na uhakika wa kunufaika na fursa za mikopo ya asilimia nne (4) kwa vijana inayotolewa na halmashauri ili kuendeleza kipato chao kitakachowainua kiuchumi.

"Serikali imekuwa ikitoa fursa za uwezeshaji kiuchumi kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Ninawaomba vijana tumieni fursa hii, azisheni vikundi vya bodaboda, visajilini, mimi nitawapeleka kupata mikopo hii ambayo haina riba," alisema.

Abood alisema kuwa kupitia mikopo watakayoipata, watakuwa na uwezo wa kununua pikipiki za kikundi vyao na kuendeleza mitaji itakayowapa mafanikio makubwa ya kijamii na kiuchumi.

"Tumieni fursa zinazotolewa na Rais wetu kwani anawapenda wananchi wake na mimi mbunge wenu nipo nitasaidia kwani tayari kuna vikundi vya bodaboda nimeshavipa pikipiki," alisema Abood.

Kuhusu zawadi za majaketi, mbunge huyo alisema kuwa mbali na kuwalinda kiusalama, pia yamebeba ujumbe wa kutangaza utalii wa nchi kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour kwa vile wanakutana na watu wa aina mbalimbali wakiwamo raia wa kigeni.

Halfan Kingama, aliyetoa majaketi hayo kwa mbunge huyo, alisema kuwa mbali na kusaidia kuzuia ajali, pia kuna lengo la kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan katika kutangaza vivutio vya Utalii vya nchini.

Madereva hao, akiwamo Ally Yusuph wa Kituo Kikuu cha Mabasi Msamvu, walimshukuru Rais pamoja na mbunge huyo kwa jitihada zao za kulijali kundi hilo.

Yusuph alisema madereva wengi wa bodaboda wamefariki dunia kwa kugongwa na magari kutokana na kukosa viakisi mwanga hivyo na upatikanaji wake kwao utasaidia kupunguza ajali barabarani hasa nyakati za usiku huku wakiutangaza utalii wa nchi.

# Wabaini mbinu mpya biashara ya binadamu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

BIASHARA ya usafirishaji haramu wa binadamu kwenye Mkoa wa Singida imeingia katika hatua mpya baada ya baadhi ya madhehebu ya dini kudaiwa kuwalaghai wazazi na kuwachukua watoto wao kwa kisingizio cha kwenda kupata elimu ya dini nje ya nchi.

Mkaguzi wa Jeshi la Polisi Kitengo cha Dawati la Jinsia Wilaya ya Singida, Amina Abdallah, aliyasema hayo juzi kwenye uzinduzi wa Wiki ya Sheria iliyofanyika kimkoa kwenye viwanja vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Singida.

"Usafirishaji haramu wa binadamu hivi sasa wengi wanakuja katika sura ya madhehebu ya dini, watoto wanachukuliwa wanakwenda kusomeshwa dini nje ya nchi," alisema.

Abdallah alisema wazazi lazima watambue kuwa ukitaka kumsomesha mtoto mambo ya dini, hata hapa nchini elimu hiyo inapatikana hadi ngazi ya chuo kikuu, hivyo hakuna sababu ya kuwasafirisha kwenda nje ya nchi.

"Eti mtoto anatolewa hapa Singida anakwenda kusomeshwa dini Uarabuni, wewe kweli unakubali kuwa dini ya kule ni nzuri kuliko inayopatikana hapa nchini? Siyo kweli!" alionya.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, aliyekuwa mgeni rasmi, alisema suala la usuluhishi ni jambo muhimu ambalo hata Rais amekuwa akisisitiza umuhimu wa kutoa haki kwa haraka.

"Tunapojadili wiki hii ya sheria, tujielekeze kwenye kutoa haki kwa njia ya usuluhishi ili tuweze kupata haki kwa haraka tuokoe uchumi wetu, lakini tuache jamii yetu wakiwa na umoja na mshikamano," alisema.

Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Singida, Allu Nzowa, alisema uzoefu wa uendeshaji shughuli za mahakama unaonyesha wananchi wengi wanapenda kutatua migogoro yao kwa njia ya kawaida ya usikilizwaji mashauri mahakamani kuliko njia ya usuluhishi.

Alisema kimsingi njia ya usikilizaji kesi mahakamani huchukua muda mrefu na gharama na kuondoa maelewano baina ya wahusika.

Septemba mwaka jana serikali ilitangaza kuanza kuchukua hatua kali za kuthibiti biashara ya usafirishaji wa binadamu nchini kwa kuanzisha kikosi kazi maalum cha kupambana na biashara hiyo ili kuziongezea nguvu taasisi zinazojihusisha na kudhibiti biashara hiyo.



# Diwani awa mbogo wazazi kutopeleka watoto shuleni

**Na Mwandishi Wetu,** BAHI

DIWANI wa Kata ya Bahi, mkoani Dodoma, Augustino Ndonu, amesema wazazi wa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023 ambao bado hawajaripoti shuleni, watachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kutozwa faini ya Sh. 50,000.

Ndonu aliyasema hayo juzi alipokuwa akitoa msaada wa vifaa vya shule kwa wanafunzi 59 kwenye kata hiyo kwa wanafunzi wanaoishi mazingira magumu.

Alisema serikali inatekeleza sera ya elimu bila malipo hivyo ni vyema wazazi wakatekeleza wajibu wao wa kuhakikisha watoto wanakwenda shule ili kutimiza ndoto zao kielimu.

"Katika halmashauri yetu kwenye mfuko wa elimu tumetoa zaidi ya Sh. milioni tatu kununua vifaa hivi ili watoto hawa wapate elimu. Leo (juzi) tumegawa shule tano zilizoko kwenye kata yetu, hivyo naagiza kuanzia leo hadi ifikapo Januari 30, 2023 watoto hao wawe wamekwisha ripoti shuleni na kuanza masomo," alisema.

Kwa mujibu wa diwani huyo, baada ya siku hizo kupita wataanza msako na kukamata wazazi wote ambao wamekaidi agizo hilo na kupeleka watoto shuleni na kulipa faini ya Sh. 50,000.

"Ni muhimu wazazi tujue faida za kusomesha mtoto hawa kwa familia zetu, tusiwaache wakakosa elimu ambayo ndo ufunguo wa maisha yao," alisema.

Naye Ofisa Elimu Sekondari wilayani Bahi, Mery Chakupewa, alisema kupitia mfuko huo wa elimu umeanzishwa na halmashauri kwa lengo la kusaidia wanafunzi wanaotoka katika mazingira magumu.

"Mfuko umewezesha wanafunzi kuwa na ufaulu mzuri katika mitihani ya shule za msingi na secondari, sababu wazazi wanatambua uwepo wa mfuko huu tuwahimize watoto kuanza shule na kumaliza," alisema.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Bahi B, Mamos Longoye, aliishukuru serikali ya wilaya hiyo kwa kuanzisha mfuko huo ambao unawasaidia watoto wanaotoka mazingira magumu kutokana na wengine kushindwa kwenda shule kwa kukosa sare na viatu vya shule.

# PIC yaipongeza EWURA kuwa taasisi ya mfano barani Afrika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), imeipongeza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa utendaji wake wa kuibuka taasisi ya mfano Afrika kiutendaji.

Akizungumza baada ya kukutana na mamlaka hiyo jana, Mwenyekiti wa PIC, Jerry Silaa, alisema EWURA inafanya kazi nzuri na tangu mwaka 2017 hadi sasa wana ithibati ya ubora kimataifa na kuibuka taasisi ya mfano Afrika.

"Ni sifa kwetu Watanzania tunapenda kujilinganisha na watu lakini wakati mwingine ziko taasisi ambazo zinatangulia mbele na watu wanakuja kujilinganisha na sisi, kwa hiyo inafanya kazi nzuri,"alisema.

Pia alisema kamati imeomba EWURA kuendelea kumlinda mtumiaji katika bei ya mafuta, gesi, umeme na maji.

"Tumeomba waongeze nguvu kwenye elimu bado kuna watu wanalalamikia kubambikiwa bili za maji. Sasa wanatakiwa kujua mahakama ya bili za maji ni EWURA, tumetaka watoe elimu kwa wananchi namna ya kufikisha malalamiko yao na kufuatilia usomaji wa mita za maji,"alisema.

Silaa alisema mamlaka za maji zilishaelekezwa kumshirikisha mteja zinaposoma mita za maji ili kujiridhishwa na kuondokana na kubambikiziwa bili. "Tunaamini taasisi hii pamoja na uongozi mzuri wa Prof. Mark Mwandosya ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi na sisi tumejifunza namna anavyosimamia vizuri taasisi hii, tumeridhika kabisa na utendaji wa taasisi hii,"alisema.




Meneja Mpango wa Taifa wa kudhibiti magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, Dk. George Kabana (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu maadhimisho ya kupambana na magonjwa hayo yatakayofanyika kuanzia Januari 30, mwaka huu kwa kuweka kambi za matibabu katika maeneo mbalimbali nchini. Wengine ni Watumishi wa Wizara ya Afya, Dk. Mohamed Nyati (kulia) na Oscar Kaitaba. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Jaji Kiongozi asisitiza kipaumbele usikilizaji wa kesi dawa za kuelvya

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu Tanzania, Mustapher Siyani, amewataka majaji kutoa kipaumbele katika kusikiliza kesi zinazohusu dawa za kulevya ili wahusika wa biashara hiyo waadhibiwe kutokana na kusababisha madhara kwa jamii.

Siyani alitoa kauli hiyo jana alipotembelea maonesho ya wiki ya sheria yanayoendelea kwenye viwanja vya Mwalimu Nyerere.

Alisema taifa linatakiwa kuchukua tahadhali kubwa kutokana na madhara ya dawa hizo.

Akiwa katika banda la Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Jaji kiongozi alisema ni vyema majaji watoe kipaumbele wakati wa kuendeshwa kwa kesi hizo.

"Mashauri ya dawa za kulevya yanaendeshwa muda mrefu mahakamani hata upelelezi haupaswi kuchukua muda mrefu kutokana na asili ya kesi hizo. Majaji toeni kipaumbele kwenye kesi hizi," alisema.

Pia aliitaka mamlaka kuelekeza nguvu zaidi kwenye kutoa elimu na kufundisha vijana kuelewa madhara.

"Kuna watu wengi mpaka leo bado hawaamini kuwa bangi ina madhara au mirungi, elimu zaidi inahitajika, kijana akipata msongo wa mawazo kidogo wa maisha anatafuta kitu cha kupotezea mawazo," alisema.

Naye Kamishna wa Sheria wa DCEA, Veronica Matikila, alisema miongoni mwa majukumu yao ni kuratibu, kukamata na kufanya upelelezi.

Alisema kuwa mamlaka hiyo hutoa uelimishaji juu ya dawa za kulevya zinavyoathiri afya, uchumi na usalama.

Katika hatua nyingine, Jaji Kiongozi alitembelea banda la Jeshi la Magereza na kuwataka kutunza vifaa vilivyotolewa na mahakama.

"Mahakama ilitoa vifaa vya kuwezesha usikilizwaji wa mashauri kwa njia ya mtandao ni jukumu lenu kutunza vifaa hivyo si tu vinaondoa gharama za kuwapeleka watuhumiwa mahakamani pia vinaokoa muda,"alisema.

Pia alisema kuwa magereza yamekuwa yakiwapa fursa wafungwa kujifunza ujuzi mbalimbali jambo linalowasaidia kujipatia kipato kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali pindi wanapokuwa uraiani.

Aidha, Jaji kiongozi alitoa wito kwa wananchi kutembelea maonesho hayo ili waweze kujifunza masuala mbalimbali ikiwamo sheria na taratibu mbalimbali kwenye mnyororo wa haki.

Ofisa TEHAMA Makao Makuu ya Magereza, Sajenti Thomas Pangani, alisema kuwa jeshi hilo ni wadau katika sheria na Magereza 18 yameunganishwa na Mahakama mtandao na kesi husikiliza bila kupeleka wahalifu mahakamani.





# Ripoti rushwa, uhujumu uchumi yaamsha matumaini ya wanasiasa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BAADHI ya vyama vya siasa vimesema taarifa ya Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) iliyotolewa hivi karibu kuhusu utendaji wa kazi wa mamlaka hiyo, imetoa mwanga wa matumaini katika kupambana na rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu taarifa hiyo, Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia Makini, Ameri Hassan Ameri, alisema ZAECA imethubutu kuchambua ripoti ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu ya Serikali Zanzibar, jambo ambalo kipindi cha nyuma halikuwapo kwa mamlaka hiyo.

Alisema mamlaka hiyo inaendelea kuifanyika kazi ripoti hiyo na tuhuma ambazo zimeelezwa kupitia Wizara ya Afya na baadaye kutoa taarifa ya waliofikishwa mahakamani kutokana na tuhuma za kuhujumu uchumi.

Alisema wanachokifanya ZAECA ni jambo la kupongezwa na kwa mujibu wa taarifa yao iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo kwa waandishi wa habari katika kipindi cha miezi minne, majadala 14 yameshafikishwa mahakamani.

Alisema mamlaka hiyo ikiendelea na kasi yake ya utendaji wa kazi, miaka michache ijayo suala la rushwa na uhujumu uchumi litatoweka.

Alisema kitendo cha ZAECA kuthubutu kurejesha fedha zaidi ya Sh. bilioni tatu zilizoibwa na wahujumu uchumi ili kuidhoofisha Zanzibar, ni cha kupongezwa.

Alisema elimu ya kupambana na rushwa inayotolewa na mamlaka hiyo itasaidia kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu masuala hayo, pia kupambana na vitendo hivyo ambavyo linaathiri taifa.

Katibu mkuu huyo aliitaka mamlaka hiyo katika kudhibiti mianya ya rushwa, ifuatilie na kufanya uchunguzi katika Jeshi la Polisi kwa kuwa kuna kesi nyingi zinaharibika mikononi mwao katika mazingira ya kutatanisha.

Hamad Muhammed Ibrahim, Katibu Mkuu wa Chama cha UPDP, alisema hatua ya ZAECA kutoka ofisini na kuwafikia wananchi katika kuwapa elimu ya rushwa, imesaidia wananchi kutoa taarifa za rushwa kwa mamlaka hiyo.

Alisema ZAECA imeanzishwa toka mwaka 2012 lakini chini ya uongozi wa Mkurugenzi Ali Abdallah Ali, kuna mabadiliko makubwa ambayo yanaifanya mamlaka hiyo kuwa karibu na wananchi.

Aliitaka mamlaka hiyo kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi hasa katika utoaji wa hukumu ili wananchi kuendelea kujenga imani kwa taasisi zinazotoa haki.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Mkurugenzi wa ZAECA kutipia kikao chake na waandishi wa habari, alisema katika kipindi cha miezi minne kutoka Septemba hadi Desemba mwaka jana, walipokea tuhuma 238 zinazohusiana na vitendo rushwa na uhujumi wa uchumi.

Kati ya tuhuma hizo, 168 zinaendelea na uchunguzi, sita zimehamishiwa taasisi zingine kwa kuendelea na hatua ikiwamo Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji, tuhuma 19 zimefanyiwa udhibiti wa kutoa elimu na tuhuma 45 zimetolewa ushauri wa kisheria.

Alisema pia majalada 18 yamefikishwa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria ikiwamo kuwafikisha mahakamani watuhumiwa.




Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha, akikabidhi ufunguo wa gari jipya aina ya Toyota Rush kwa mkazi wa Kahama, Samson Daniel, baada ya kuibuka mshindi wa kampeni ya "Ndinga la Kishua", jijini Dar es Salaam juzi. Washindi wengine akiwamo wa Sh. milioni 20 na Sh. milioni 10 walikabidhiwa fedha zao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi ajivunia maboresho huduma za uwanja wa ndege

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema uamuzi wa serikali kushirikiana na kampuni zenye hadhi duniani, umesaidia kuboresha huduma kwenye Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume na kuuweka katika hadhi ya juu ya viwango vya kimataifa.

Aliyasema hayo visiwani hapa juzi alipozindua huduma za uwanja huo (Terminal 3) na kuruhusu mashirika makubwa yanayotoa huduma uwanjani huko kuanza kazi.

Alisema hivi sasa serikali anayoiongoza inajivunia mafanikio makubwa katika uimarishaji wa huduma za uwanja huo ikiwamo ongezeko la safari za moja kwa moja (direct flights) za mashirika mbalimbali ya ndege za kimataifa.

Alisema mashirika ya ndege yapatayo 34 yanafanya safari zake kwa kutumia uwanja huo na kwa sasa kuna ongezeko kubwa la watalii na abiria kwa kutumia usafiri wa anga na kupitia kwenye jengo la abiria Terminal 3.

Dk. Mwinyi alisema katika mwaka 2022, idadi ya abiria ilifikia milioni 1.8 kulinganishwa na milioni 1.3 kwa mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 38.

Alisema kuwa baada ya kufanyika kwa mabadiliko makubwa ya shughuli za uwanja huo, mapato yameongezeka kutoka Sh. bilioni 6.7 kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba na kufikia Sh. bilioni nane kwa kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Desemba mwaka jana.

"Hili ni ongezeko kubwa kuwahi kutokea. Ongezeko la safari za ndege na abiria limepelekea kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar," alisifu.

Dk. Mwinyi aliongeza: "Ninatoa shukrani kwa wizara, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Kampuni ya Dnata, Emirate Leisure na Segap na wadau wote wa Sekta ya Anga kwa ushirikiano wao mzuri katika kuimarisha huduma zinazotolewa kwenye kiwanja hiki.

"Ni imani yangu kwamba mtaendeleza jitahada hizi ili tuweze kufikia viwango tunavyotarajia."

Rais alizitaka taasisi zinazotoa huduma kwenye uwanja huo kutoa huduma katika viwango cha kimataifa, hatua ambayo itaongeza ushawishi kwa mashirika mengine makubwa ya ndege kutoa huduma za safari za moja kwa moja Zanzibar.

Alisema ubora wa huduma za uwanja wa ndege ndiyo sura itakayowezesha mashirika mengine na taasisi kufungua huduma zake baada ya kuridhishwa na mazingira yaliyoko.

Dk. Mwinyi pia aliitaka Idara ya Uhamiaji kuongeza ufanisi wa majukumu yake katika kutoa huduma kwa wageni wanaoingia kwenye uwanja huo, wakiwamo watalii, kwa kupunguza msongamano na usumbufu unaojitokeza.

Rais Dk. Mwinyi alitumia nafasi hiyo kuipongeza kampuni ya Dnata inayotoa huduma kwenye uwanja huo kwa kuanza kwa kasi yenye mwelekeo mkubwa wa matumaini ambapo jumla ya ajira za vijana 600 zimepatikana.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed alisema mikakati ya serikali ni kuifungua Zanzibar katika sekta ya miundombinu ya anga ambapo mipango hiyo iko katika hatua za mwisho za kuanza kwa ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba kuwa wa kimataifa.

Alisema kipindi cha nyuma utoaji wa huduma kwenye uwanja huo haukuwa wa kuridhisha kutokana na upungufu mkubwa wa vifaa na zana za kisasa za kufanyia kazi na pamoja na ucheleweshwa wa utoaji wa huduma kwa abiria na mizigo.

Alisema pia kulikuwa na changamoto za vitendo vya rushwa, upotevu wa makusanyo ya mapato na upotevu wa mizigo ya abiria.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Dnata Group, Steve Allen, alisema wamejipanga kuongeza ubora wa huduma zao kwa ajili ya kukidhi malengo na matarajio ya kuyawezesha mashirika makubwa ya ndege ya kimataifa kufanya safari zake Zanzibar moja kwa moja.

Steve ambaye ni Mwenyekiti Mtendaji wa Kampuni ya Emirate Leisure Retail na MMI, alisema Zanzibar sasa inatengeneza ukurasa mpya wa historia ya visiwa vyake kwa kuimarika vivutio vya utalii kupitia huduma bora wanazozitoa viwanjani huko.

Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Miundombinu ya Usafirishaji ya Baraza la Wawakilishi, Yahya Rashid, alisema kuanza kazi kwa Terminal 3 kunaimarisha huduma za anga kwa Zanzibar na kupokea idadi kubwa ya watalii.



# TABASAMU LA USHINDI

MWIMBAJI maarufu wa Injili nchini, Rose Mhando ni kama amefufuka upya baada ya wimbo wake mpya 'Secret Agenda' kufanya vizuri.

Wimbo huo ambao kwa sasa umetawala anga la muziki kwa kuchezwa kila kona, unatokana na safari ndefu iliyojaa furaha na machungu baada ya kupotea katika tasnia ya muziki.

Jina la Rose Mhando lilikuwa maarufu miaka ya 2000 baada ya kutoa nyimbo kadhaa zilizowachemsha mashabiki wake hapa nchini na Afrika Mashariki kwa ujumla.

Mabadiliko aliyoyafanya kwa kuchanganya muziki wa kuchezeka, ilisababisha muziki wa Injili kubadili mwelekeo kutoka kuwa kutoa huduma zaidi na kuwa kuburudisha.

Historia ya maisha ya Rose Mhando imejaa machungu mengi kutoka magonjwa hadi madai ya matumizi ya dawa za kulevya, lakini yote amepambana nayo mpaka sasa amerudi tena akiwa na nguvu mpya.

"Machungu yangu niliyoyapitia nilibeba mengi ya watu wengine, ukiwa na uchungu unabeba moyo wa kijikataa ni ngumu kujikubali na ndivyo niliweza kuishi," Rose amesema wakati akihojiwa katika kipindi cha Hard Talk.

Pamoja na kutamba na nyimbo nyingi kama 'Nibebe' na Nipe Uvumilivu', lakini maisha yake yalitawaliwa na upweke na sononeko kutoka kwa watu waliomzunguka.

Wimbo wa 'Secret Agenda' ni kama umemrejeshea tabasamu la ushindi katika mapito yaliyojaa machungu.

Amesema mwaka 2023 amepanga kufanya mambo mazuri zaidi na kwamba mashabiki wake wazidi kumwombea ili Mungu azidi kumpatia nguvu ya uimbaji.

BASI SAWA

## Farby atikisa Mapenzi Bongo

NYOTA wa muziki wa kizazi kipya, Abdallah Said maarufu Farby, ameachia ngoma yake 'Mapenzi', ikiwa ni jitihada za kutaka kupenya katika soko la muziki nchini.



Akizungumza na BT, Farby amesema video ya wimbo huo imeanza kuchezwa na kufungua rasmia njia ya mafanikio kisanaa anayoyapigania.

Amesema ingawa kuna ushindani mkubwa kutokana na ubora pamoja na wingi wa wasanii, lakini hiyo inaongeza mwamko na nguvu zake katika hali ya kupigania mafanikio yake kisanaa.

"Nimefanikiwa kuachia wimbo wangu unaokwenda sambamba na video yangu iliyoanza kuonekana katika vituo vya televisheni pamoja na chaneli ya mtandanoni," amesema.

## Basila apongezwa kwa ujasiri

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Basila Mwanukuzi, amepongezwa kutokana na ukomavu wake alionyesha baada ya jina lake kutokuwapo katika orodha ya viongozi waliobaki katika nafasi hiyo.

Basila ambaye alikuwa mshindi wa shindano la Miss Tanzania na mwanamitindo, baada ya kuachwa kwenye nafasi hiyo katika mkeka uliotoka juzi, aliandia ujumbe mrefu ambao ulimpongeza na kumshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kumpa majukumu mazito na kumheshimisha katika jamii.

Katika ujumbe huo, Basila amesema kuwa japokuwa kuna wanawake na vijana wengi mahiri wenye uwezo na weledi, lakini alimwona na kumpa heshima na dhamana ya kuwa Mkuu wa Wilaya ya Korogwe.

Ujumbe huo ambao ulionekana kuandika kwa ukomavu ulipongezwa na mashabiki zake ambao wengi walimtia moyo na kumtaja kama mwanamke jasiri na anayetambua umuhimu wa dhamana ya uongozi.





## MADAM RITA AZITAKA LEBO KUCHANGAMKIA

MWANZILISHI wa shindano la Bongo Star Search, Madam Lita, ameshangaa wamiliki wa lebo za muziki kutowachukua wasanii wanaoibuliwa na shindano hilo.

Amesema wao kama BSS hawataki pesa yoyote endapo lebo itamchukua msanii anayetoka katika shindano hilo kama wanavyofanya nchi zingine.

"Nashangaa wamiliki wa lebo wanashindwa kuja kuwachukua wasanii tunaowaibua kama wanavyofanya nchi zingine, nawaomba waje kuwaangalia na kuwasainisha, sisi hatutaki chochote kama watakubaliana," amesema Madam Rita.





## Kingereza cha Harmonize chawakera wengi

MWANAMUZIKI wa kizazi kipya, Harmonize amewakera mashabiki zake baada ya kuzungumza Kiingereza badala ya Kiswahili katika ziara yake nchini Rwanda.

Katika mahojiano yake na kituo cha Televisheni cha Rwanda, mwanamuziki huyo licha ya kuulizwa kwa Kiswahili safi na mtangazaji, yeye alijibu maswali kwa kutumia lugha hiyo kiasi ambacho kimeonekana kuwakera wengi.

"Harmonize anatakiwa kujitathmini au uongozi wake umpatie ushauri namna ya kutumia lugha katika mahojiano yake, mtangazaji wa Rwanda alionekana kufurahia Kiswahili yeye anajifanya kuzungumza Kingereza ni mbaya sana," amesema Rajabu ambaye alitoa maoni baada ya mahojiano hayo.

## MWAMBA HUYU HAPA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuzitazama filamu nyingi za Kizungu, Kihindi, Kikorea, Kichina na hata Kinigeria zenye lugha ya kwao kwa miaka mingi, mwanzoni mwa miaka ya 1990 vijana wengi wa Kitanzania walipata fursa ya kuanza kuzisikia zikitafsiriwa kwa Kiswahili.

Filamu nyingi za miaka ya mwanzoni ya 1970 hadi mwishoni mwa miaka ya 1980 ambazo zivuma mno, zilianza kutafsiriwa kwa Kiswahili na kuzidi kuzipa umaarufu.

Hata zile mpya zilizotoka miaka ya 1990 hadi sasa zimekuwa zikitafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, hivyo kuleta mvuto na kupendwa na Watanzania wengi kwa sababu wanakuwa wanakifahamu kinachozungumzwa na maudhui ya filamu yenyewe.

Kwa sasa hata tamthilia zimekuwa zikitafsiriwa kwa lugha adhimu ya Kiswahili.

Leo tutawaangalia Watanzania maarufu ambao wamekuwa wakiweka maneno ya Kiswahili kwenye picha hizo

**Mkandala Lufufu**

Anaitwa Kepteni Dereck Gasper Mukandala Lufufu. Huyu ndiye mwanzilishi au mwasisi wa kutafsiri filamu za nje ya nchi kwa lugha ya Kiswahili hapa Tanzania. Ni kepteni wa Jeshi la Wananchi mstaafu ambaye alifariki dunia 2015 jijini Dar es Salaam na kuacha majonzi makubwa kwa watu wengi wapenda filamu na tamthilia, hasa ikikumbukwa kuwa ndiyo wakati tasnia hiyo ilikuwa inakuwa kwa kasi biashara hiyo ikichanganya sana kutokana na kukua kwa teknolojia, lakini watu wengi kuwa na uwezo wa kumiliki TV.

Hakuna kijana au mtoto yeyote wa miaka ya 1990 mpenda picha ambaye hamtambui. Watoto waliomba pesa kwa mama zao na kwenda kwenye vibanda vya video maarufu kama 'vibanda umiza' kwenda kuangalia filamu alizoweka maneno ya Kiswahili kama yeye mwenyewe alivyokuwa akisema, hasa ikizingatia wakati huo bado nyumba nyingi zilikuwa hazina TV. Nakumbuka wakati huo kiingilio ilikuwa ni Sh. 50/- tu.

Alitafsiri filamu za aina zote kwa umahiri mkubwa, lakini anakumbukwa kwa mbwembwe, kuiga sauti za wahusika wote ndani ya filamu, awe mwanaume, mlevi, aliyejeruhiwa kwa kupigwa, mwanamke mtu mzima, msichana, tajiri, maskini, kila mmoja alimtafutia sauti yake na ikawa burudani tosha. Alitengeneza maneno na misamiati mingi kwenye filamu zake kama 'kukotola' (kukimbia), 'kanyampasila', (rumande), 'kanyabazongo (kizunguzungu), bastola aliita 'mguu wa kuku.' Hakuwa mtafsiri tu, bali ni mshereheshaji 'muvi'. Jamaa ana mambo mengi sana ambayo unaweza kumaliza makaratasi yote kumwelezea. 'Akamwaga mwaaani' akiwa na maana akaanza kupiga risasi.

**Juma Khan**

Ndiye mtafsiri anayependwa zaidi na mashabiki wengi wa picha za Kihindi zilizotafsiriwa kwa Kiswahili. Hii inatokana na labda kufahamu vizuri lugha hiyo kwa ufasaha kutokana na utundu wake, pamoja na kupitia mikononi mwa watu wenye asili hiyo wakati akitafuta mafanikio kwenye kazi hiyo.

Pamoja na hayo, huyu jamaa amekuwa akiweka nakshi nyingi na mbwembwe zilizovutia wengi, ikiwamo misemo kadhaa.

Msemo ni 'mwamba huyu hapa', umebuniwa na mwamba huyu na mpaka sasa unatamba kwenye nyanja mbalimbali za michezo, hususan mpira wa miguu na burudani. Ni msemo ambao kwa sasa umetawala kila kona.

Juma Khan au Chikongwe hana mpinzani kwenye hili kwa sababu mashabiki wengi wa filamu hizo, wanasema picha yoyote ya Kihindi iliyotafsiriwa kwa Kiswahili kama aliyefanya kazi hiyo siyo huyo basi ni kama pilau bila kachumbari.

**DJ Msati**

Huyu naye anatafsri sana filamu za Kihindi na tamthilia zake, anakuja juu kwenye kazi hiyo. Ni mmoja wa watafsiri anayejizolea mashabiki wake kila kukicha ambaye ni maarufu kwa jina na 'baba la baba.'

**DJ Murphy**

Ni mtafsiri kutoka Arusha ambaye anatafsiri picha zote za Kizungu, Kikorea, Kijapani na nyingine nyingi. Naye amejizolea sifa kubwa kutokana na aina yake ya kutafsiri akiwa na sauti nzito kuliko yeye mwenyewe alivyo.

FILAMU

## Usiku wa Balaa: Hukumu bila ushahidi

**Na Adam Fungamwango**

NI kweli ilikuwa usiku wa balaa. Usiku ambao ulikuwa ni mshikemshike kwa familia mbili ambazo zilikuwa hazijuani. Zinajikuta zikiingia kwenye matatizo makubwa ambayo hayakusababishwa na wao.

Filamu inaitwa 'Usiku wa Balaa' na kweli ilikuwa hivyo. Imechezwa na Betrice Urio, Mohamed Fungafunga, Mzee Jangua, Batrice Jaffet, Nurat Chuma, Hussein Shomari na wengineo.

Awali haikuonekana kama tatizo linaweza kuwa kubwa kiasi hicho. Ram alikimbizwa na vibaka usiku akiwa katika harakati za kurudi nyumbani.

Baada ya kuona kuwa atauawa akaingia moja kwa moja kwenye nyumba ya mtu na moja kwa moja akajificha uvunguni.

Mwenye nyumba hiyo alikuwa ameacha mlango wazi amekwenda kuoga. Alikuwa ni mke wa mzee Jengua. Kabla Ram hajatoka uvunguni na kujikabidhisha kwa mama mwenye nyumba, baba mwenye nyumba alipiga hodi. Akafunguliwa na kuingia.

Jamaa kule uvunguni akaona sasa itakuwa ngumu kutoka na kuongea chochote akaeleweka. Akaendelea kujificha uvunguni.

Mke wa Ram naye akaona usiku umekuwa mwingi, akapiga simu ili kujua mumewe yuko wapi. Simu ikawa inaita, lakini haipokelewi.

Ile simu sasa ikawa inaita chini ya uvungu wa kitanda cha mzee Jengua. Wote wakasikia, lakini mzee Jengua ndiye aliyeshtuka zaidi.

Akawa anatafuta wapi simu inaita. Kule uvunguni jamaa alijitahidi kila njia ili simu isiiite mpaka akafanikiwa kuizima.

Mkewe huku nyumbani presha juu, kwanza simu ilikuwa inaita haikupokelewa, halafu baadaye imezimwa. Akajua moja kwa moja yuko kwa mahawara zake. Akaangua kilio. Mzee Jengua machale yakamcheza. Mwishowe akaamua atazame uvunguni. Sura yake ikakutana ana kwa ana na kijana Ram. Hakuna kiswahili hapo. Moja kwa moja ikaonekana kuwa alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mkewe, hivyo amewafumania.

Ugomvi ukawa mkubwa sana, kama unavyomjua mzee Jengua (marehemu). Ilikuwa ni patashika nguo kuchanika. Akapigiwa simu mke wa Ram kuwa mumewe amefumaniwa. Ilibidi aje hadi pale na kuhadithiwa kila kitu alivyokuwa uvunguni.

Ndoa zote mbili zilivunjika. Lakini baada ya siku chache tu, mzee Jengua anakutana na Ringo na kumhadithia jinsi kijana mmoja alivyonusurika kuuawa na vibaka akaamua kuingia nyumba jirani karibu na kwake. Alipomuuliza nguo alizovaa zilikuwa ni zile zile alizomfuma nazo Ram.

Papo hapo akaona kumbe haikuwa kweli alivyodhani na amefanya kosa. Akaenda kwa mkewe kumuomba msamaha. Halafu akakutana na mke wa Ram na kumwambia ukweli wote jinsi ilivyokuwa, akisema alihukumu bila ushahidi kwa sababu alimkuta uvunguni mwa kitanda. Ndoa ya Ram na mkewe nayo ikarejea upya.




# Yemi Alade umempata hadi rais



MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Yemi Alade, ameamua kuwacheka watu wanaoeneza uvumi kwamba ana ujauzito wa Rais wa Togo, Faure Essozimna Gnassingbé Eyadéma.

Mwimbaji huyo iliseme-kana kuwa na uhusiano wa kimapenzi na kiongozi huyo na kuwa na ujauzito wake.

Uvumi huo ulianza pale mwanadada Tosin Silver-dam, alipoingia kwenye ukurasa wake na kusam-baza video ya mwanamume mmoja akidai kuwa Yemi Alade ni mjamzito wa rais wa Togo na ana mpango awe mke wake wa sita.



## Lilian kumbe ulichachuka zamani?

MWIGIZAJI kutoka Nolly-wood, Lilian Afegbai, amefichua kuwa nusura afukuzwe chuo kikuu baada ya kupiga picha za ngono katika filamu na Jim Iyke.

Afegbai akizungumza kwe-nye kipindi cha Tea with Tay, alisema alikabiliwa na uamuzi wa kamati ya nidhamu katika Chuo Kikuu cha Benson Idahosa (BIU) cha nchini Benin.

Alisema tamasha la uigizaji lilikuwa jukumu lake la kwanza la sinema wakati huo alikuwa akichanganya masomo ya shule na taaluma ya filamu.

"Nilianza kuigiza kikamilifu nikiwa BIU. Katika filamu ya kwanza niliyoifanya, karibu wanifukuze shule kwa sababu nilikuwa na picha ya kuhamasi-sha ngono ndani ya Jim Iyke". Amesema.

## Kylie Jenner amtambulisha mtoto wake

BAADA ya takriban mwaka mmoja, Kylie Jenner ametam-bulisha jina la mtoto wake wa kiume na kuweka picha zake hadharani.

Mtoto huyo wa kiume ni wa pili kwa Jenner na Travis Scott.

Jenner aliweka picha yake kwenye Instagram yenye neno "Aire," akidokeza kwamba ni jina la mtoto huyo.

Jenner awali alimpa mtoto wake jina la Wolf. Baadaye alisema kwamba jina hilo hali-kuwa sawa kwake na kwamba alikuwa akilibadilisha.





## Chris ala bata Kenya

STAA wa uigizaji wa Austral-ia, Chris Hemsworth anaye-julikana kwa kuigiza katika filamu ya 'Extraction' ame-fanya ziara nchini Kenya.

Hemsworth aliweka picha zake na familia yake ka-tika mtandao wa Instagram wakifurahia katika mbuga ya kitaifa nchini Kenya.

Muigizaji huyo anaelezea safari yake nchini humo ni ya kukumbukwa zaidi.

"Mojawapo ya safari ya ku-kumbukwa sana Kenya familia yangu na mimi kuwahi kuwa nayo," ameandika Hemsworth.

## 2Baba alilia kutokomezwa unga

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Innocent Idibia, anayejulikana kama 2Baba, ametoa wito kwa Wakala wa Kitaifa wa Kudhibiti Sheria ya Dawa za Kulevya (NDLEA) kuimarisha vita dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya wakati nchi inapojiandaa kwa uchaguzi ujao.

2Baba, ambaye ni rais wa taasisi ya kupambana na matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana, amesema ni muhimu kupambana na wau-zaji na wasambazaji wa dawa hizo katika kipindi cha uch-aguzi ili kuweka utulivu.

Ameongeza kuwa dawa za kulevya, zimesalia kuwa kichocheo kikuu cha ghasia za uchaguzi na aliomba lazima zifutiliwe mbali kabla na baada ya uchaguzi.





## Wajasiriamali wadogo kuwezeshwa mitaji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAJASIRIAMALI wenye mitaji midogo katika Soko la Samunge, jijini Arusha, wanatarajia kunufaika na mkopo wa Sh. milioni 110 uliotolewa na Nabii Mkuu wa Kanisa la Ngurumo ya Upako, Geor Davie.

Akizungumza jana kwenye soko hilo, baada ya kutembelea na kuongea na wajasiriamali hao, Geor Davie alisema ametoa Sh. milioni 100 na anamshukuru Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, kwa kumuunga mkono kwa kutoa Sh. milioni 10.

Pia alisema kabla ya kufika hapo alipokea barua ya maombi ya wajasiriamali hao wakiomba kuongezewa mitaji yao kutokana na wengi wao kuyumba baada ya kuunguliwa na soko hilo mwaka 2019.

"Sasa nilipata barua hiyo nilitoa hundi ya Sh. milioni 50 lakini nilipofika hapa nimebadili mawazo na nimeongeza tena Sh. milioni 50 na nimeamua kutoa Sh. milioni 100 ili kuwasaidia wahitaji maana nimeona uhitaji ni mkubwa," alisema.

Aliomba Sh. milioni 80 itolewe kwa watu wenye uhitaji hasa wale wenye mitaji midogo ili kuinua biashara zao, huku Sh. milioni 20 ipelekwe kwenye uwekezaji wa magari imara ya soko hilo.

"Watu wenye uhitaji wapo wengi kuiachia serikali pekee haiwezi bali na sisi viongozi wa dini yatupasa kurudisha sadaka tulizokusanya miaka na miaka kutoka kwa waumini kwa njia ya kuwapatia mitaji ili nao wainuke kiuchumi.

"Msaada huu ninaotoa naamini watu wataongeza mitaji yao na naomba watu wasibaguliwe bali kila mmoja apewe kwa kadri itakavyowezekana nipo hapa kusaidia jamii na naomba niletewe majina ya hao wafanyabiashara niwaombee," alisema.

Mbunge Gambo alisema katika soko hilo, wajasiriamali wanakabiliwa na matatizo mbalimbali baada ya soko lao kuungua moto mwaka 2019 na kukosa msaada wa mtu yeyote.

Alitaja baadhi ya matatizo wanayokabiliana mayo ni ukosefu wa mitaro, majengo na usumbufu wa migambo.

"Kuna baadhi ya mambo niliyafanya sokoni hapa ikiwamo kusaidia kuchimba kisima cha maji na nilitoa Sh. milioni 20 kwa kinamama 100 lakini leo natoa Sh. milioni 10," alisema.

# RC azibana halmashauri fedha za lishe

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, ameagiza wakurugenzi wa halmashauri katika mkoa kutenga na kutoa Sh. 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano ili kusaidia utekelezaji wa mpango wa afua za lishe na udhibiti wa udumavu.

Nyerere aliagiza hayo jana wakati wa kikao kazi cha utekelezaji wa mkataba wa lishe, uliotekelezwa kati ya Julai hadi Desemba, mwaka jana.

"Wakurugenzi wote mnatakiwa kutoa Sh. 1,000 kwa kila mtoto ili kusaidia afua za lishe,"alisema.

Nyerere alisema ili mkoa ufikie malengo yake, idara ya afya inatakiwa kuimarisha tiba, huduma za lishe, huduma za wajawazito na watoto na kusimamia ubora wa lishe.

Pia alisema fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya afua za lishe zitumike mpaka Juni, mwaka huu na taarifa zifike ofisini kwake juu ya utekelezaji wa suala hilo.

"Suala la lishe ni muhimu sana. Unaweza ukakuta mtoto ni mtulivu na hakosi darasani lakini kumbe amedumaa na ambaye ni mtukutu anafanya vizuri darasani kumbe hajadumaa,"alisema.

Awali Ofisa Lishe wa Mkoa wa Manyara, January Dalushi, akizungumza katika kikao hicho, alisema kwa mujibu wa utafiti wa kitaifa uliofanyika mwaka 2018, udumavu katika mkoa wa Manyara ni asilimia 36.1.

Ofisa lishe huyo alisema halmashauri zingine hazijafikia kiwango kinachopangwa kutolewa cha Sh. 1,000 kwa mtoto mmoja.

Dalushi alisema ili kutekeleza vizuri mkataba huo wa lishe, jambo la muhimu ni kupanga bajeti ya lishe kwenye vyanzo vya fedha vyenye uhakika kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Akichangia mjadala huo, Ofisa Mipango na Uratibu wa Mkoa, Maarufu Mkwaya, aliwaomba wakurugenzi kutenga Sh. 1,000 kwa watoto na wanapozitenga waangalie wanazipeleka wapi.

Pia Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa anayeshughulikia Afya, Dk. Damas Kayera, alisema hawatapitisha bajeti ya lishe kama halmashauri hazitazingatia maelekezo ya serikali.

Dk. Kayera alisema hivi karibuni watafanya tathmini ya lishe ili kubaini udumavu kwa mkoa huo kama umepungua kwa kuwa wanatumia takwimu za nyuma.

Naye Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Adam Mhako, alisema wana uhaba wa vitendea kazi katika vipimo na hawana kipimo cha ukondefu kwa watoto.

Mhako alisema kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, mwaka jana, waliwapatia nyongeza ya matone ya vitamin A watoto 29,209.




Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Barrick Gold Corporation, Mark Bristow, akikabidhi mfano wa hundi ya dola 10,000 za kimarekani kwa mwakilishi wa asasi isiyo ya kiserikali ya Hope for Girls and Women Tanzania, Rhobi Samwelly, kwa ajili ya kusaidia shughuli za asasi hiyo katika hafla iliyofanyika mkoani Shinyanga juzi. Kulia ni Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge aokoa jahazi watoto waliokwama kidato cha kwanza

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MBUNGE wa Monduli, mkoani Arusha, Fredy Lowassa, amelipatia ufumbuzi wa haraka, tatizo la wanafunzi 200 wa jamii ya kifugaji ya Kimasai waliokuwa wamekwama kujiunga kidato cha kwanza mwaka huu wilayani humo, kutokana na kukosa mahitaji muhimu zikiwamo sare za shule.

Pia amesema ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia duniani na mabadiliko ya tabianchi, jamii za kifugaji hazina budi kubadili mtizamo na kuwekeza katika elimu kwa watoto badala ya kukumbatia ufugaji wa mifugo mingi.

Akizungumza juzi wilayani humo wakati akikabidhi magodoro, masanduku, madaftari, sare za shule na mahitaji mengine, alisema kwa hali ilivyo sasa ni lazima jamii hiyo ibadilike na kujikita zaidi kuwapa elimu watoto wao.

"Leo (juzi) tunashindana kuhusu mifugo hakuna ujanja kwa sababu watu wanaongezeka ardhi haiongezeki ni kweli tumekuwa tukiamini kuwa mifugo ndio benki yetu, lakini kwa hali ilivyo sasa haiwezekani,"alisema Lowassa.

Lowasa alisisitiza kuwa jamii hiyo ya kifugaji ndiyo inahitaji elimu zaidi kuliko jamii nyingine yoyote na kutokana na mfumo wa maisha yao, ambayo tangu wamezaliwa wanakua kwa kuona mifugo, jambo ambalo kwa sasa haliwezekani kutokana na binadamu kuongezeka huku ardhi ikibaki ile ile.

"Tunachojua ni mifugo tu sababu dunia inabadilika hakuna kitu muhimu kama elimu tulinde heshima ya elimu kwa wilaya ya Monduli. Sisi kama jamii ya kifugaji tuna changamoto kubwa zaidi. Sisi ndio tunatakiwa kufahamu umuhimu wa elimu kuliko mtu mwingine yeyote,"alisema.

Pia aliwataka wananchi wa Monduli kuenzi mawazo ya Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, ambaye ni mwasisi wa shule za kata nchini kwa kuwatendea haki watoto wa jamii ya Kimasai kwenda shuleni.

"Naomba mfahamu nafasi ya Monduli kwenye elimu ya Tanzania. Monduli ndiyo kitovu cha elimu Tanzania nzima. Monduli ndio tulianzisha shule za kata nchi nzima ambazo wakati ule ilikuwa jambo gumu sana na jambo hili lilisimamiwa kutokea Monduli.

"Mnafahamu nani alisimamia ni mzee Lowassa, lakini alipata mate na baraka za ardhi hii ya Monduli, sasa kama mlimpata mtu yule mkamtuma duniani akaenda akahubiri elimu, halafu sisi tunashindwa kuishi hiyo elimu itakuwa aibu kubwa sana,"alisema .

Baada ya makabidhiano hayo, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Ole Sokoine, Thomas Lukumay, alisema licha ya mwamko mkubwa wa elimu kwa wazazi, tatizo la ukame limeathiri familia nyingi kutokana na idadi kubwa ya mifugo kufa.

"Karibia asilimia 35 ya wanafunzi waliopangiwa kujiunga kidato cha kwanza wameshindwa kuripoti shule kutokana na kukosa vifaa vya shule wazazi wengi wanapiga simu kuomba muda wa kuendelea kufanya maandalizi," alisema Lukumay.

Alimshukuru Lowassa kwa kuwasaidia watoto hao waliokwama kwenda shuleni kwa sababu ya ukosefu wa vifaa vya shule.

Baadhi ya wanafunzi waliopata msaada huo Mustapha Simon ambaye amepangiwa kwenda Shule ya Sekondari Engutoto alimshukuru mbunge huyo kwa msaada huo.

"Hapo awali nilikuwa nahuzunika nikiona wenzangu wanaenda shule sababu mimi siwezi. Lakini sasa mbunge kanirudishia matumaini nitaenda shule na ninahidi kusoma kwa bidii," alisema Mustapha.

MAKALA

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# ZAMA ZILE HUDUMA ZA UGAWAJI...

## - Maisha kwa maduka ya kaya, kila kitu foleni, kuwahi nafasi kwa kupanga jiwe

**Na Adam Fungamwango**

SIKU moja nilikuwa nazungumza na baba yangu maongezi ya kawaida tu. Akaniambia enzi zao wao kabla na baada ya Uhuru chai inapikwa nyumbani halafu unatumwa sukari dukani. Na dakika mbili unarudi kutoka dukani unampa mama sukari na chai inanyweka.

Mimi nikacheka. Akauliza unacheka nini. Nikamjibu ya kweli hayo baba? Naye akaniambia kuwa huwezi kuamini kwa sababu nyinyi watoto wa sasa mmeanza kupata akili kipindi zama nyingine zimechukua nafasi, bidhaa hizo adimu, kuzipata dukani bahati nasibu na majaliwa yake, Mungu ndiye anayejua; hakuna sukari, unga, mchele wala sabuni madukani. Hiyo ilishika kasi miaka ya 1970 hadi mwishoni mwa mwazoni mwa mwaka 1986.

Hili lilichangiwa sana na kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa nchi za Tanzania, Kenya na Uganda na baadaye Vita ya Kagera.

Vita ya Kagera ilipiganwa kati ya Tanzania kuanzia Oktoba 30 mwaka 1978 hadi Aprili 11, 1979, kugombea mkoa wa Kagera ambao Rais wa Uganda wakati huo, Idd Amin Dada alidai, mto Kagera na baadhi ya ardhi ya mkoa huo ni mali yake.

Tanzania iliibuka kidedea kwenye vita hiyo kwa kuichakaza Uganda. Hata hivyo vita ni vita. Iliacha makovu pamoja na uchumi kuyumba, kiasi cha Wabongo kutangaziwa 'kufunga mikanda'.

Hali ya chakula ikaanza kuwa mbaya, kiasi kwamba hakuna aliyekuwa mtoto, kijana au mzee wa kati huo ambaye leo yupo hai akakosa kukumbuka hali hiyo.

Mbali na uhaba wa chakula. Kulikuwa pia na uhaba wa mahitaji mengine kama sabuni, dawa za meno, miswaki na vitu vingine vingi ambavyo nitakuja kuvielezea siku kwenye safu hii.

Ukawekwa utaratibu ili wananchi wote wapate, unga huo ukawa haupelekwi kwenye maduka ya kawaida ya watu binafsi. Yakaundwa maduka ya ushirika. Kila wananchi wa eneo fulani walikuwa wakijiorodhesha majina chini ya viongozi wao ambao ni wajumbe wa nyumba kumi na kufungua duka. Haya ndiyo yaliyokuwa yakiitwa maduka ya kaya.

Nia ilikuwa nzuri, lakini tatizo utelekezaji wake ukawa mbovu kiasi yakafa kifo cha asili.

Kila mtu anaandikisha kama ana mke na idadi ya watoto alionao. Wenye watoto wengi walipata kilo nyingi za unga kuliko wenye watoto wachache. Na unga pamoja na bidhaa zingine kama mchele au sukari, mafuta ya taa, siku vikija, vinauzwa kwa kufuata reja iliyopo. Kama ulipata wiki hii, basi mpaka wiki ijayo. Ukimaliza chakula chako mapema utajua mwenyewe. Rushwa kama kawaida ilikuwapo. Wauzaji pamoja na baadhi ya wajumbe wa nyumba kumi hawakuweza kutowapatia wanakaya mahitaji yao wakati mwingine kwa kuwarusha hata wiki tatu, huku unga, mchele au sukari wakiwauzia watu wengine kwa kiasi kikubwa cha pesa, kilichoitwa mwendo wa kuruka. Hali hii wakati mwingine ilisababisha mzozo mkubwa. Kali kuliko yote wakati mwingine wanakaya wanalazimishwa, ukinunua unga, mchele au sukari ni lazima ununue na maharage, kibiriti, au kunde. Yaani ni lazima ununue na bidhaa ambayo wao wanaona haiuziki kwa urahisi au haina wateja wengi.

Hayo maharage yaliyokuwa yanauzwa kwa lazima ni yale ambayo hayakuwa yanaiva kwa urahisi. Wakati mwingine ni lazima yatiwe magadi.

Wakati huo huo kulikuwa na magari yaliyokuwa yakisambaza chakula, kama unga, mchele, sukari yaliyoitwa Magari ya Ugawaji, siku yakipeleka kwenye maduka binafsi ambapo inakuwa ni kwa nadra sana, foleni yake inakuwa si ya kawaida. Kuna watu wanaweka mawe, makopo kama foleni kuanzia alfajiri. Wakati mwingine kunakuwa na ugomvi, patashika nguo kuchanika ili mradi tu kila mmoja anataka yeye awe wa kwanza kupata.

Magari ya Ugawaji yakionekana tu, basi watu wanayafukuza ili kuona wataishia duka gani. Watu waliwahi kufukuza hadi gari la maiti wakidhani ni la ugawaji.

Miaka mingi baadaye, hasa katikati ya miaka ya 1990 ndiyo nilianza kumwelewa kwa sababu nilianza kuyaona kwa matendo sasa.

Ni kwamba bidhaa zilianza kuonekana madukani na ilikuwa ni kweli sasa kinamama walikuwa wanatutuma sukari dukani wakati chai imeinjikwa. Mwanzoni ilikuwa ni kama miujiza hivi, lakini baadaye ikazoeleka.

Haya ni matukio yaliyotokea huko nyuma hapa nchini ambayo hayatafutika na kubaki kama kumbukumbu kwa vizazi vingi vijavyo kuona Tanzania ilipokuwa wakati mwingine inapitia vipindi vigumu.

Kwa sasa kuna baadhi ya vijana wanaona kama vile nchi ina matatizo ya uchumi, lakini wangewauliza wakubwa wao wangewaambia kilichotokea mara baada ya kumalizika kwa Vita ya Kagera. Na wangewaambia watoto wa vijana wao kuwa kulinganisha na kipindi kile cha mpito, hivi sasa wananchi wa Tanzania wanaishi maisha ya raha sana. Ni pesa yako tu. Kipindi kile hata ukiwa na pesa unaweza kulala njaa na hasa mijini, hususan Dar es Salaam. Angalau hata vijijini ungeweza kupata walau mihogo, mahindi, ndizi na vyakula vingine.

Kizazi ambacho kilikutana na hali hiyo ambacho bado kipo, waliangalia na hali ya sasa, pamoja na kusikitika, wakikutana na kusimulia vimbwanga walivyokuwa wanakutana navyo.

Baadhi ya wadau waliniambia visa, pamoja na changamoto walizowahi kukutana nazo, mmoja wao ni huyu.

"Enzi hizo mgambo waliokuwa wanalinda kwenye maduka ya kaya walikuwa wanaabudiwa sana mitaani kwani wao kila ukija mgao na wao hawakosi kupewa, tofauti na watu wa kawaida ambao wao ni mpaka yao ifike. Wauzaji wa maduka haya walikuwa hawajui kabisa kubembeleza wateja kwani wateja walikuwa hawana uchaguzi kutokana na kutakiwa kununua mahitaji yao kwenye maduka walikoandikishiwa." Mwingine akaniandikia.

"Ilikuwa ni kawaida kupita kwenye maduka na kukuta msururu mrefu wa mawe yaliyopangwa kama alama ili wenye mawe hayo wakija wapate nafasi ya mbele kwenye foleni. Nakumbuka kulazimishwa kununua unga wa muhogo wenye mchanga ili tuweze kupata sukari kilo mbili na nusu kwa mujibu wa kadi yetu ya duka la kaya iliyokuwa inayonyesha kwamba nyumba yetu ina wanakaya watano."

Watu walifunguka haswa kwenye mada hii, mwingine akaandika.

"Duh, kweli umenikumbusha mbali. Nakumbuka kijijini kwetu kulikuwa na mama aliyekuwa muuzaji katika lile duka letu la Ujamaa alikuwa ndiyo staa pale kijijini. Tulikuwa tunasubiria mafuta ya taa au kiberiti."

"Yale mawe na madebe matupu yaliyochakaa tulikuwa tunayaita 'mabandika', tuliuziwa kwa nguvu mbaazi ambazo zilikuwa hazivi, watu badala ya kuuziwa unga kwa kilo wakawa wanauziwa mahindi kwa kilo sasa jiulize ukienda kusaga kilo tatu za mahindi.

Nimekunywa sana uji wa chumvi, maana mgao wetu sisi ulikuwa kama kilo mbili hivi, wakati mwingine hazitufikishi hata wiki." Akaandika mdau mwingine.




Hizi ni baadhi ya chapa za bidhaa za madukani zilizokuwa maarufu sana miaka ya 1970, lakini zikaadimika mwishoni mwa miaka hiyo na zingine zilianza kurejea miaka ya 1990. Kwa asilimia kubwa chapa za bidhaa hizi ambazo ni dawa, sabuni, viberiti kwa sasa hazipo tena.

## Russia yazidi kuitwanga Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

JESHI la Ukraine limesema kuwa hatari ya mashambulizi ya anga ya Russia imeendelea kuwa ya juu, wakati ikizidisha kuipiga nchi hiyo kwa makombora ya ndege zisizo na rubani.

Mashambulizi hayo yaliongezeka siku moja baada ya makombora na ndege zisizo na rubani za Russia kuwaua watu wapatao 11 ikiwa ni katika kujibu hatua ya washirika wa Magharibi kuahidi kuipatia nchi hiyo vifaru.

Russia pia imefanya mashambulizi 37 ya anga, 17 yakiwa kwa kutumia ndege zisizo na rubani aina ya Shahed zilizotengenezwa Iran.

Jeshi la Ukraine limesema limedungua makombora 47 ya Russia kati ya 59.

Wakati huo huo, Shirika la Kimataifa la kudhibiti matumizi ya Nishati ya Nyuklia, IAEA, limesema mashambulizi yamesikika karibu na kinu cha nyuklia cha Zaporizhzhia.

Waziri Mkuu wa Hungary, Viktor Orban, alisema kuwa nchi yake itapinga vikwazo vyovyote vya Umoja wa Ulaya dhidi ya Russia ambavyo vinaathiri nishati ya nyuklia.

**DW**

## Bomu lawaua watu 40 Nigeria

**ABUJA,** NIGERIA

IDADI ya watu waliokufa katika shambulizi la bomu dhidi ya kundi la wafugaji katikati ya Nigeria imefikia 40.

Gavana wa Jimbo la Nasarawa, Abdullahi Sule, alisema jana kuwa idadi hiyo imeongezeka kutoka ya awali ya watu 27, waliouawa katika shambulizi lililotokea siku ya Jumatano huko Rukubi, kijiji kilichoko kwenye mpaka wa majimbo ya Nasarawa na Benue.

Sule alisema shambulizi hilo lilisababishwa na ndege isiyokuwa na rubani ambayo ilidondosha bomu, bila ya kutoa maelezo zaidi nani aliyekuwa akiiendesha ndege hiyo.

Chama cha wafugaji, kilisema bomu hilo lilidondoshwa na ndege ya kijeshi ya Nigeria.

Wakulima na wafugaji katikati ya Nigeria wamekuwa wakizozana kuhusu haki za malisho na maji kwa miongo kadhaa, lakini ghasia zimeongezeka katika miaka ya hivi karibuni baada ya baadhi ya wakulima kujiunga na magenge ya uhalifu ambayo yanavamia vijiji.

**DW**

## Mahakama yaamuru mwanamke kumlipa fidia mwanaume

**KAMPALA,** UGANDA

MWANAMKE mmoja nchini Uganda ambaye aliumiza moyo wa mchumba wake, ameamrishwa na mahakama kulipia hasara za kifedha kwa uchungu wa kisaikolojia aliosababisha.

Mahakama ya Kanungu iliamuru Richard Tumwine kulipwa shilingi milioni 9.4 za nchi hiyo, kutokana na kumsomesha mwanamke huyo aliyefahamika kwa majina ya Fortunate Kyarikunda, katika ngazi ya shahada ya uzamivu.

Hakimu Asanasio Mukobi, alisema kuwa Kyarikunda alikiuka ahadi na kusababisha madhara kwa Tumwine.

Mahakama ilisema kuwa isiyo na maana, upotoshaji na ulaghai aliyofanya mshtakiwa kudai kuwa wazazi wake walimwambia asiolewe na mwanaume mzee.

Haijulikani iwapo Kyarikunda atakata rufani dhidi ya hukumu.

Wakosoaji walisema gazeti la Monitor kwamba hukumu ina kasoro kwa sababu uchumba ni tofauti na ndoa ambayo inakubalika kisheria.

# Waasi M23 wateka mji mwingine muhimu

**GOMA,** DRC

WAASI wa M23 wanadai kuuteka mji muhimu wa Kitchanga ulioko eneo la Masisi Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo baada ya siku tatu za mapambano makali.

Mashirika ya kiraia na majeshi ya Umoja wa Mataifa nchini DRC yamelaani mashambulizi ya waasi hao, ambayo yamesababisha raia laki nne kuyakimbia makazi yao. Redio ya Okapi inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa iliripoti kuanguka kwa Kitshanga kwa waasi hao.

Picha za mamia ya watu walioikimbia mji huo zilisambazwa kwenye mitandao ya kijamii.

"Ndiyo sasa tuna Kitshanga na vitongoji vyake", msemaji wa M23 Willy Ngoma aliambia BBC jana.

Wakati wa kuanguka kwa Kitchanga, seneta wa DRC, Francine Muyumba, alitoa wito kwa bunge kuketi kwa kikao cha dharura kwa sababu nchi yao inafanya vibaya.

Mchakato wa amani wa Luanda uliomba M23 kusitisha mapigano na kujiondoa katika maeneo ambayo imeyateka, lakini waasi hao wengi wao wakiwa wa kabila la Kitutsi, walisema wameingilia kati kukomesha mauaji mengine ya kimbari dhidi ya Watutsi.

Kitshanga ni mji muhimu ulio katika njia ya mwisho iliyo wazi kati ya vitovu vikuu vya kiuchumi Kivu Kaskazini vya Goma na Butembo.

Kwa miaka kadhaa, Kitshanga imekuwa ngome na makao makuu ya kiongozi wa waasi maarufu Laurent Nkunda na kundi lake la waasi la CNDP, ambalo baadaye lilikuja kuwa M23.

Kabla ya kuuteka, waasi hao walikabiliwa na upinzani mkali kutoka wanajeshi wa serikali, wakati walipokata mawasiliano muhimu ya mji mkuu wa eneo la Goma.

Polisi na maofisa wa eneo hilo walithibitisha kuwa kundi hilo linaloongozwa na Watutsi lilikuwa limekata barabara kati ya Kitchanga na Goma.

Barabara kuu inayoelekea kaskazini kutoka Goma imekatika tangu M23 walipovamia.

**BBC**



Waombolezaji wakiwa wamebeba miili ya Wapalestina wakati wa maziko katika mji wa Ukingo wa Magharibi wa Jenin. **PICHA: VOA**

# Wapalestina 9 wauawa kwenye uvamizi

**YERUSALEM,** PALESTINA

MAJESHI ya Israeli yamewaua Wapalestina wasiopungua tisa, akiwamo mwanamke mwenye umri wa miaka 60 na wengine kadhaa kujeruhiwa.

Kulingana na maofisa wa afya wa Palestina, mauaji hayo yamefanywa wakati wa uvamizi eneo linalokaliwa kimabavu katika Ukingo wa Magharibi.

Ghasia zilitokea wakati maofisa wa afya wa Palestina walichoelezea kuwa ni operesheni kali ya mchana katika kambi ya wakimbizi ya Jenin, ambayo ni ngome ya wanamgambo wa Ukingo wa Magharibi ambayo imekuwa ikilengwa kwa kwa takriban mwaka mzima. Mzozo uliongezeka mwezi huu, huku Wapalestina 29 wakiuawa tangu kuanza kwa 2023. Haikufahamika mara moja watu wangapi kati ya wale waliouawa Alhamisi walikuwa na uhusiano na makundi yenye silaha. Mapigano yamekuja wiki kadhaa baada ya serikali mpya ya Israel ya mrengo wa kulia kuingia madarakani.


Serikali hiyo iliahidi kuchukua msimamo mkali dhidi ya Wapalestina na kuimarisha ujenzi wa makazi ya walowezi katika ardhi za Wapalestina wenye matumaini ya kuwa na taifa lao. Mapigano hayo pia yamekuja siku kadhaa kabla ya ziara ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, ambaye anatarajiwa kuwasili katika eneo hilo na kushinikiza hatua zinazoweza kuboresha maisha ya kila siku kwa Wapalestina.

Jeshi la Israel lilisema lilikuwa likifanya operesheni zake za nadra nyakati za mchana kwa sababu lilipokea taarifa za kijasusi kwamba kundi la wanamgambo lilikuwa limepanga mashambulizi dhidi ya Waisraeli.

**VOA**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**GERALD KANIUS GERALD** anatangaza kupotea kwa RESULT SLIP ya kidato cha nne yenye index namba **S3224-0458** iliyotolewa na baraza mitihani la Taifa kupitia **SAKU SCONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/MBA/RB/36793/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMED MZEE BARAKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 248 CVL – TVS KING.** Chassis namba **MD6M14PA2M4A08941.** Engine namba **AK4AM4108357.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya Polisi: DAR/OST/RB/36759/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PASTORY MAKOYE NCHEYE.** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 962 BLA** aina ya **NISSANI.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya polisi.
**KAH/RB/79/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ALLY RIZIWAN WAZIRI** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 721 DKS - TVS KING**. Chassis namba MD6M14PA3N4B01811. Engine namba **AK4B114901315.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya Polisi:
**DAR/CEN/RB/34280/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

NDUGU **KULWA MAENDELEO KAJORO** inatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye jina la BEE SAFARI COMPANY LIMITED nayenye namba za usajili **T666CNT** aina ya TOYOTA PRADO, Rangi Nyeusi yenye Engine No. **2TR0954811** na Chasis No. **TRJ1500011642** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba **DSM/PHQ/RB/31435/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**UPENDO ANDERSON LEMA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 888 DXG – SUBARU IMPREZA.** Chassis namba **GE 2002215.** Engine namba **EL 15D638010**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CHA/RB/10931/2023.**

## OFISI ZA MATANGAZO

***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya kijiji nchini ambacho kipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na umbali huo, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja wa wasichana warembo katika kijiji hicho anayepata shida hiyo. Hawana mahali kwa kupeleka malalamiko, wala wa kumlalamikia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# MTAKE MSITAKE-16

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**




WANAKIJIJI hao ambao walionekana kuchoshwa na umaskini mkubwa walioupata na wanaoendelea kuwa nao baada ya asilimia 70 ya ardhi yao kuchukuliwa, walinyamaza wamsikilize ofisa huyo.

"Baada ya kuona hakuna dalili za ujenzi wanakijiji mlianza kuhoji na kuongea bila woga kuonyesha kutoridhishwa na hilo.

Viongozi waliokuwa wamepewa mlungula na mwekezaji wakaa tena kikao, wakaona wawaongopee wanakijiji kwa kuwapa pesa kama wanakodisha. Mwekezaji sasa akaanza kuwatumia wanakijiji hao hao kama vibarua.

Ujanja uliotumika ni kwamba aliwapa kila mtu pesa kidogo, halafu ni kama alikuwa amewarudisha kila mmoja ardhi aliyokuwa akiimiliki ili waendelee kulima, lakini mazao alikuwa akiyachukua mwenyewe na kwenda kuyauza Dar es Salaam na mikoa akijipatia pesa nyingi na kuwalipa pesa ndogo. Ndivyo, sivyo?"

"Ndiyo mheshimiwaaa."

"Baada ya mwaka mmoja mwingine ndipo mlipoanza kuona athari ya walichofanya, kaanza kulalamika, lakini badala ya kujibu hoja yoyote aliyeonekana kupinga alishughulikiwa. Liliundwa kundi kama sungusungu, kazi ilikuwa ni kukamata, kuadhibu, kumtesa na kumuua yeyote yule anayeonekana kidomodomo wa kutaka kuwazindua watu."

Kwa hali ilivyokuwa hapo, kila mtu sasa alijua Mheshimiwa Mosha Usonzo siku zake za kuwepo uraiani zinahesabika. Ni mtu ambaye licha ya kuwanyang'anya ardhi na kuwatia umasikini, lakini aliwatesa na kuwaua baadhi ya wanakijiji, hasa wale waliokuwa wakihoji baadhi ya mambo yaliyooneka kwenda vibaya.

"Sasa ni hivi wananchi, baada ya uchunguzi wa kina, kutoka kwa watu wa Makao Makuu, Dar es Salaam na mkoani, tumegundua hili na hapa mnapotuona tumekuja kusafisha kila kitu na kuanzia sasa tumetengua ununuzi wote na kila kitu kilichofanywa na yeye. Ardhi yote inarudishwa kwa wanakijiji..." Kabla hajamaliza, kelele za shangwe vilivyoambatana na

**"Amri imetoka tena Makao Makuu kuwa Mwenyetiki wa Kijiji naye akamatwe, ila wajumbe tu ndiyo wasiguswe." Kelele za shangwe zilisikika tena.**

kwenda sambamba na vigelegele vya kinamama vilisikika kwa dakika zaidi ya mbili.

Sehemu hiyo sasa haikuwa ni ya burudani, hafla au sherehe, kama ilivyokuwa mwanzo, bali iligeuka kuwa ni mkutano wa kijiji kizima, kwani hata wale ambao hawakuwepo hapo walijikongoka kila mmoja kujua mustakabali wao, baada ya kupata taarifa kuwa maafisa wa serikali toka mkoani wamefika kwenye kijiji hicho kiichoonekana kama kimesahaulika.

"Wananchi tusikizane, tafadhali. Mimi kama mmoja wa maafisa, nasema kila mwanakijiji kesho akachukue eneo lake ambalo lilinunuliwa au kuchukuliwa kwa hila la mwekezaji wetu feki huyu. Pia yeye mwenyewe kuanzia sasa yupo chini ya ulinzi na tutaondoka naye hapa kwenda mkoani tukafuate taratibu zote kisheria, kabla ya kumpeleka Dar es Salaam kwa hatua zaidi za kisheria."

Wanakijiji hawakutaka kusikiliza hata maneno mengine, ile kusema tu yupo chini ya ulinzi, tayari iliwafanya washangilie kwa nguvu na wengine kuanza kupiga ngoma na kucheza kwa mbwembwe zote.

Wakati afisa yule akiongea maneno hayo, askari wawili walishuka kwenye moja kati ya magari waliyokuja hayo na kwenda moja kwa moja kwenye jukwaa kuu na kumzingira Usonzo.

Walimwamuru asimame. Akatii. Wakamfunga pingu. Halafu akaongozwa kwenda kwenye gari.

Kila kitu kiligeuka. Awali ilikuwa ni sherehe au hafla. Ilikuwa maalum kwa kumuaga Adel. Kijana huyo aliyefika hapo zaidi ya miezi sita sasa kwa ajili ya kumchukua bibi yake mgonjwa, lakini akajiingiza kwenye mapenzi na msichana Mary kiasi cha kuwamgiwa tindikali iliyomfanya kuwa kipofu. Kwa wanakijiji walijua kuwa yeye mwenyewe ameamua kuondoka. Lakini nyuma ya pazia ni kwamba alishawishiwa na Usonzo na Mary. Akaambiwa kuwa anapelekwa kwenye Hospitali ya Muhimbili akatibiwe na huendsa akapona.

Upande wa tatu kwa Usonzo na Mary ulikuwa ni mpango wa kumuondosha hapo kumpeleka Hospitali ya Muhimbili ili wakamtelekeze, halafu na wao watorokee jijini Arusha.

Haikuwa hivyo tena, Usonzo amekamatwa. Sauti ikasikika tena.

"Amri imetoka tena Makao Makuu kuwa Mwenyetiki wa Kijiji naye akamatwe, ila wajumbe tu ndiyo wasiguswe." Kelele za shangwe zilisikika tena.

Afisa yule aliyekuwa kwa DJ na MC, bado aliendelea kuongea maneno ambayo kwa asilimia zote yaliwafurahisha wanakijiji cha Maweni.

"Wakati tunaendelea na hili, sisi kama maafisa wa serikali, tumesikitishwa sana na kitendo kilichotokea huku cha mmoja kati ya wageni kwenye kijiji chenu kumwagiwa tindikali kiasi cha kupofuka macho. Nimesema kila kitu nilichokuwa kinafanyika huku kuna watu walikuwa wanatupa taarifa humu humu kijijini. Kwa maana hiyo yoyote aliyefanya hivyo ni lazima hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake. Na kama tulivyojua kila kitu kuhusu uwekezaji feki wa Usonzo, tunamjua aliyefanya hivyo, wala hatutaki kumuuliza mtu, tuna ushahidi wote. Tunajua kuwa kijana huyo yupo hapa na tunamuomba aje huku kwenye kipaza sauti ili tumuulize mswali kadhaa mbele yenu, kabla ya kumkataba mhusika."

Hapa kidogo wanakijiji walibaki kimya. Kila mmoja alikuwa anajua ya Mary ndiyo aliyefanya hivyo. Na amekiri mbele ya hafla hiyo kabla ya maafisa hao kufika. Kila moja alikaa makini kuona nini kinatokea.

Adel alinyanyuka na kumuacha Mary pembeni yake aliyekuwa amejiinamia. Alianza kujikokota na kujipeleke mbele akitumia fimbo yake kupapasa. Alikuwa amevaa shati lake jeusi, suruali ya bluu na viatu vyeusi, akipiga mawani yake myeusi pia. Safari hii hakuongozwa na Mary kama ilivyokuwa kawaida ya wanakijiji walivyozoea. Akafika kwenye jukwaa la MC na DJ wake, akapewa kipaza sauti kingine kwa ajili ya maswali.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# UWANJA MPYA WA GEITA GOLD KUKAMILIKA MEI

**Na Mwandishi Wetu**

UWANJA wa mpira wa miguu wa Magogo unaojengwa na Halmashauri ya Mji wa Geita kwa kushirikiana na Kampuni ya Geita Gold Mine Limited (GGM), unatarajiwa kukamilika Mei mwaka huu.

Kwa mujibu wa Makamu wa Rais wa AngloGold Ashanti anayeshughulikia miradi endelevu ya Ghana na Tanzania, Simon Shayo, awamu ya kwanza ya ujenzi wa uwanja huo unaojengwa katika eneo la Magogo, Kata ya Bombambiliipo mbioni kukamilika.

Shayo alitoa taarifa hiyo baada ya kuulizwa waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa mchezo kati ya Geita Gold FC na Coastal Union ya Tanga ambapo matokeo yalikuwa 1-0.

Alisema wanajenga uwanja bora na salama kwa watumiaji na kwamba kazi hiyo inafanyika kwa ufanisi ikisimamiwa na mshauri ambaye, ameajiriwa na halmashauri ili ashauri namna ya kumalizia awamu ya kwanza na nyingine.

"Kwa kushirikiana na halmashauri na uongozi wa mkoa wa Geita, nia yetu kuhakikisha hadi kufikia Mei mwaka huu uwanja uwe umekamilika na kuanza kutumika," alisema Shayo.

"Kwa hiyo hii itategemea sana kasi ya makandarasi wetu na wote tunaofanya nao kazi ambao tunaamini kwamba watahakikisha uwanja huu unakamilika kwa wakati, kwani nia yetu ni kuwa na uwanja bora," alisema.

Aliongeza kuwa hawataki kufanya kwa kuikimbiza na kuwa na eneo ambalo watu wanaweza kupata majeraha au uwanja ambao unaweza kuwa na dosari siku zijazo.

"Kama mjuavyo sisi kipaumbele chetu cha kwanza ni usalama, kwa hiyo tungependa kuona wachezaji na mashabiki wanafanya shughuli zao kwenye uwanja ambao ni salama."

Aidha, akizungumzia udhamini wa zaidi ya Sh. milioni 800 ambao kampuni hiyo ya GGML imetoa kwa Klabu ya Geita, Shayo alisema sasa anaona timu inafanya vizuri.

"Tumeona timu inafanya vizuri, tulishuhudia wachezaji walivyocheza mechi zilizotangulia, tumeambiwa wanazidi kusomana na kadiri timu inavyokaa pamoja tunaamini kwamba itaendelea kuimarika zaidi," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Zahara Michuzi, akizungumzia ujenzi wa uwanja huo na faida zake alisema utazidi kufungua fursa za kiuchumi kwa wananchi wa mkoa wa Geita.

Awamu ya kwanza ya ujenzi wa uwanja huo inakadiriwa kuwa Sh. bilioni 2.4 ambazo zimetolewa na GGML kwa asilimia 80 kupitia mpango wake wa uwajibikaji kwa jamii, ikishirikiana na Halmashauri ya Mji wa Geita.



Mwonekano wa uwanja wa mpira wa miguu wa Magogo unaendelea kujengwa utakaotumiwa na Timu ya Geita Gold FC. **PICHA: GGM**

# *Shindano la Waitara Golf kutimua vumbi leo Lugalo*

**Na Saada Akida**

SHINDANO la kumuenzi mwasisi wa klabu ya Jeshi ya Gofu ya Lugalo na Mkuu wa Majeshi Mstaafu, George Waitara (Waitara Golf Tournament), yanayodhaminiwa na kinywaji cha Johnnie Walker linatarajiwa kutimua vumbi leo.

Shindano hilo litafanyika kwenye Klabu ya Gofu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Lugalo jijini Dar es Salaam.

Wachezaji zaidi ya 100 kutoka klabu mbalimbali za mchezo huo wa gofu hapa nchini wamethibitisha kushiriki shindano hilo hilo linalofanyika kila mwaka.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Klabu ya Lugalo, Meja Selemani Semunyu, alisema maandalizi yapo vizuri na klabu kutoka Tanzania Bara na Visiwani zimethibitisha kushiriki na ziko tayari kwa shindano hilo la leo.

Alizitaja baadhi ya klabu hizo zitakazocheza leo ni Dar es Salaam Gymkhana, Morogoro Gymkhana, Arusha Gymkhana, TPC , Moshi Club, Mufindi na Zanzibar.

"Kila kitu kuhusu shindano hilo kinaenda vizuri katika kuhakikisha tunaendelea kumuenzi mwasisi wetu huyo na tuna imani yanafanyika kwa weledi mkubwa na kutakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu ya wachezaji wamejiandaa vizuri," alisema Semunyu.

# Mkwawa Queens yasajili 6 kuepuka kushuka

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mkwawa Queens kutoka Iringa inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa soka la wanawake, imesajili wachezaji sita wazoefu kwa ajili ya kuisaidia kusalia kwenye ligi hiyo.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miraji Fundi amesema kuwa wachezaji hao wamesajiliwa kwenye kipindi cha dirisha dogo lililofungwa hivi karibuni, akiongeza kuwa anaamini watakisaidia kikosi kupambana kwa ajili ya kusalia kwenye Ligi Kuu.

"Lengo letu msimu huu ni kubali Ligi Kuu. Baada ya kutofanya vema, tumeongeza wachezaji sita ambao ni wazoefu na sasa wapo mazoezini wameonyesha nia ya kutufanyia kazi hiyo," alisema Fundi.

"Unajua timu hii imepanda daraja msimu huu, tuna wachezaji wadogo tu ambao hawakuwa na uzoefu wowote, siku zote Ligi Kuu siyo kama Ligi Daraja la Kwanza wachezaji walikuwa hawajazoea ligi na wamekutana na ugumu na ubora wa wachezaji wa timu pinzani. Ukiangalia timu nyingi kwa sasa zina wachezaji kutoka nje ya nchi, sasa wanapata shida kidogo, lakini watazoea," aliongeza Fundi ambaye ni kocha mwanzilishi wa soka la wanawake Tanzania, akiifundisha Sayari Queens katikati ya miaka ya 1990.

Aliwataka mashabiki wa soka Iringa kujitokeza kwa wingi Februari Mosi kwenye Uwanja wa Mkwawa, kuishangilia timu hiyo ambayo itacheza dhidi ya Baobab Queens.

Mkwawa Queens ndiyo timu inayoburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi moja tu, ikicheza mechi sita mpaka sasa, ikiwa haijashinda mechi yoyote, ikitoka sare moja na kupoteza mechi tano, hivyo kukabiliwa na janga la kushuka daraja mwishoni mwa msimu.

Kwenye Ligi ya Soka Wanawake, timu mbili za mwisho hushuka daraja mwishoni mwa msimu na nyingine mbili zitapanda Ligi Kuu.

Timu hiyo yenye maskani yake Iringa, ilipanda msimu huu pamoja na timu ya Amani Queens ya Lindi ambaye yenyewe ina pointi nne kwenye nafasi ya nane.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### OSIMHEN ATAKIWA MAN
KLABU ya Manchester United inaweza kutoa ofa ya pauni milioni 105 kwa mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen, lakini uhamisho wa mshambuliaji huyo wa Nigeria mwenye umri wa miaka 23 huenda hautafanyika hadi msimu wa joto. (***Soccer News***)

### GUSTO KUBAKI LYON
CHELSEA huenda ikalazimika kuchelewesha mipango ya kumsajili beki wa kulia wa Ufaransa, Malo Gusto mwenye umri wa miaka 19 Januari huku rais wa Lyon, Jean-Michel Aulas akisema anatarajia mchezaji huyo kusalia Ufaransa hadi angalau msimu wa joto. (***Football London)***

### PORRO AKARIBIA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur ina imani kuwa dili la mlinzi wa Sporting Lisbon na Hispania, Pedro Porro litakamilika siku zijazo baada ya ugumu wa mazungumzo kuhusu kipengele cha kuachiliwa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. (***90min***)

### LAMPTEY AULIZIWA BRIGHTON
KLABU ya Sporting Lisbon wameuliza kuhusu kupatikana kwa Tariq Lamptey wa Brighton mwenye umri wa miaka 22 kuchukua nafasi ya Pedro Porro, huku Lyon pia ikimtaka beki huyo wa pembeni wa Ghana. ***(90min)***

### GORDON KUPUNGUZWA BEI
EVERTON wanatarajiwa kupunguza bei yao ya pauni milioni 60 kwa winga wa England, Anthony Gordon mwenye umri wa miaka 21 na kukubali karibu pauni milioni 40 pamoja na nyongeza baada ya hesabu yao ya awali kukataliwa na Newcastle United. (***Telegraph***)

### MCKENNIE AKARIBIA LEEDS
LEEDS United iko tayari kulipa pauni milioni 25 kwa Juventus na kiungo wa kati wa Marekani, Weston McKennie mwenye umri wa miaka 24. (***Sky Sports Italy***)

### ZANIOLO SASA BOURNEMOUTH
KLABU ya Bournemouth wana nia ya kumsajili kiungo wa kati wa AS Roma na Italia, Nicolo Zaniolo mwenye umri wa miaka 23, huku uhamisho wao wa kumnunua mshambuliaji wa Villarreal na Senegal, Nicolas Jackson mwenye umri wa miaka 21, ukionekana kama umegonga mwamba. (***Mail***)


### MILAN KUACHANA NA NICOLO
AC Milan pia inataka kumsajili Nicolo Zaniolo, lakini inavutiwa na mshambuliaji wa Ufaransa na Newcastle, Allan Saint-Maximin kama mbadala wake. (***Sky Sports Italy)***

### DUMFRIES AGOMBEWA ULAYA
CHELSEA, Newcastle United na Manchester United zote zinavutiwa na mlinzi wa Uholanzi na Inter Milan, Denzel Dumfries, huku Inter ikiweka bei ya euro milioni 40 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. (***Gazzetta dello Sport)***

### DIAZ AIKUBALI ROVERS
MSHAMBULIAJI wa Blackburn Rovers, Ben Brereton Diaz amekubali kujiunga na klabu ya Hispania, Villarreal msimu wa joto kwa uhamisho wa bure. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile mwenye umri wa miaka 23 mkataba wake unamalizika pale Ewood Park mwishoni mwa msimu. ***(Mail)***

### SOARES SAFI FULHAM
FULHAM imeripotiwa kukubali mkataba wa mkopo kwa beki wa pembeni wa Arsenal na Ureno, Cedric Soares mwenye umri wa miaka 31. (***90min)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BENZEMA ATAKA MABAO YA MAPEMA REAL MADRID

## ●●● Ni baada ya kutoka nyuma na kuitoa Atletico kwenye robo fainali ya Copa del Rey, huku...

**MADRID,** Hispania

KARIM Benzema amedokeza kwamba, Real Madrid lazima watafute mabao ya mapema katika michezo yao kama hawataki kuteseka baada ya kutoka nyuma na kushinda 3-1 dhidi ya Atletico Madrid kwenye Copa del Rey.

Los Blancos walishindwa kuzifumania nyavu hadi robo saa ya mwisho ya muda wa kawaida katika dimba la Santiago Bernabeu, huku Rodrygo akisawazisha bao la kwanza la Alvaro Morata.

Kusawazishwa kwa bao hilo kulilazimisha timu hizo kwenye muda wa ziada katika mchezo wa robo fainali Alhamisi, huku mabao yaliyoipa ushindi Real Madrid yakifungwa na Benzema na Vinicius Junior.

**Mshindi huyo wa tuzo ya Ballon d'Or alikiri kuwa timu yake haikuwa sawa katika muda wa kawaida, lakini akasisitiza kila mara walikuwa na ubora wa kujibu.**

"Ulikuwa mchezo mgumu na mgumu sana," alisema mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

"Lakini kwa wachezaji na vipaji tulivyonavyo, tulijua tunaweza kurejea mchezoni.

"Pengine tunahitaji kufunga mabao mapema, kwa sababu hatupendi kuteseka. Atletico walijiweka vizuri, wakaingia na hilo lilitugharimu. Bao la kusawazisha la Rodrygo lilitupa nguvu kubwa."

Bao la Vinicius liliihakikisha Real kumaliza usiku mgumu na kutinga nusu fainali ya kombe hilo.

Kocha Carlo Ancelotti alimsifu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 katika maoni yake baada ya mechi.

"Vinicius amekuwa akitaka kucheza na alikuwa akizingatia sana mchezo," alisema.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,069,8
MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
READING
1 | 1.16
X | 6.54
2 | 13.78
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LAMPARD ALIVUNJA UKIMYA BAADA YA KUTIMULIWA



**LONDON,** England

FRANK Lampard amewashukuru mashabiki wa Everton na kuipongeza "klabu maalum yenye moyo mkubwa," baada ya kutimuliwa mapema wiki hii.

Lampard alifukuzwa Jumatatu baada ya kichapo cha 2-0 kutoka kwa West Ham, ambacho kiliiacha Everton katika nafasi ya 19 kikiwa pointi sawa na Southampton inayoshika mkia.

Mfungaji bora wa Chelsea, Lampard alijiunga na Everton Januari mwaka jana, akichukua nafasi ya Rafael Benitez - mtu asiyependwa na mwenye mgawanyiko kati ya mashabiki wa Toffees hao.

Lampard aliunda uhusiano na mashabiki wa Everton, lakini alikuwa kwenye hatari ya kushuka daraja.

Hata hivyo, ushindi mara tatu mfululizo kutoka katika mechi sita za mwisho za Everton ziliwafanya wanusurike na ushindi wa 3-2 dhidi ya Crystal Palace katika uwanja wa Goodison Park ukiwahakikishia kuendelea kwao kubaki Ligi Kuu.

Wameshinda mara tatu pekee kwenye ligi na Lampard akawa kocha wa sita kutimuliwa na mmiliki wa klabu hiyo, Farhad Moshiri tangu kuwekeza katika klabu hiyo mwaka wa 2016.

Siku ya Alhamisi, Lampard alituma ujumbe wa kwaheri kwenye akaunti yake rasmi ya Instagram na taarifa hiyo pia ikishirikiwa na Chama cha Wasimamizi wa Ligi (LMA).

"Nilipokuja Everton mwaka jana nilijua tulikuwa katika wakati mgumu na siku zote nitajivunia kazi ya ajabu na uungwaji mkono kutoka kwa kila mtu aliyehusika kuibakisha timu katika Ligi Kuu msimu uliopita," aliandika Lampard.

"Shukrani kwa kila mtu ambaye alicheza jukumu lake wakati klabu nzima ilikusanyika. Sitasahau usiku wa ajabu dhidi ya Palace ambao tulishiriki.

"Nataka kuwashukuru wana Everton wote kwa makaribisho mliyonipa mimi, wafanyakazi wangu na familia yangu. Hakika ni klabu maalum yenye moyo mkuu na historia ya ajabu.

"Nimesikitishwa kwamba hatukuweza kufikia zaidi pamoja na kuwatakia wachezaji wote na kila mtu katika Everton FC mema zaidi kwa siku zijazo."

Lampard, ambaye alikaa chini ya mwaka mmoja tu akiongoza, alishinda mechi tisa pekee kati ya 38 za Ligi Kuu, kumaanisha asilimia yake ya ushindi (23.7) ni bora kuliko ile ya Mike Walker (19.4).

# Toure afukuzwa Wigan kwa kukosa ushindi

**LONDON,** England

KOLO Toure amefukuzwa kazi katika Klabu ya Wigan Athletic chini ya miezi miwili baada ya kuinoa klabu hiyo inayoshiriki Ligi ya Championship nchini England.

Toure, beki wa zamani wa Arsenal, Manchester City na Liverpool, aliteuliwa kuwa kocha wa Wigan Novemba 29.

Ilikuwa kazi yake ya kwanza kwenye ukocha.

Hata hivyo, Toure mwenye umri wa miaka 41 alifukuzwa kazi Alhamisi baada ya siku 59 za kuiongoza timu hiyo na kushindwa kushinda mechi yoyote kati ya tisa.

Wigan ya Toure ilipoteza mechi sita kati ya hizo na kukaa mkiani mwa msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 25 katika mechi 28.

Mtendaji mkuu wa Klabu hiyo, Malachy Brannigan alisema: "Kwanza, ningependa kumshukuru Kolo kwa juhudi zake wakati wake katika klabu yetu.

"Kwa bahati mbaya, matokeo uwanjani hayajakuwa vile tulivyopenda na uamuzi mgumu kama ulivyokuwa, Bodi iliona ni muhimu kuachana nae na kujipanga upya."



861,169/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/01/23 | 18:00 | Hull City vs Queens Park Rangers | 2.50 | 3.30 | 2.70 |
| 02. 28/01/23 | 18:00 | Blackburn Rovers vs Birmingham City | 2.27 | 3.20 | 3.15 |
| 03. 28/01/23 | 23:00 | Getafe CF vs Real Betis Seville | 2.95 | 2.95 | 2.55 |
| 04. 29/01/23 | 14:15 | FC Twente Enschede vs Feyenoord Rotterdam | 2.75 | 3.45 | 2.40 |
| 05. 29/01/23 | 15:00 | OGC Nice vs Lille OSC | 2.95 | 3.30 | 2.35 |
| 06. 29/01/23 | 15:30 | RSC Anderlecht vs Royal Antwerp FC | 2.75 | 3.25 | 2.50 |
| 07. 29/01/23 | 16:00 | Real Valladolid vs Valencia CF | 3.10 | 3.25 | 2.28 |
| 08. 29/01/23 | 16:30 | Brighton & Hove Albion vs Liverpool FC | 2.65 | 3.50 | 2.45 |
| 09. 29/01/23 | 17:00 | AJ Auxerre vs Montpellier HSC | 2.45 | 3.30 | 2.80 |
| 10. 29/01/23 | 17:00 | Clermont Foot 63 vs FC Nantes | 2.37 | 3.30 | 2.90 |
| 11. 29/01/23 | 17:30 | Schalke 04 vs 1. FC Cologne | 2.95 | 3.40 | 2.29 |
| 12. 29/01/23 | 18:00 | Cercle Brugge vs KAA Gent | 3.05 | 3.30 | 2.29 |
| 13. 29/01/23 | 18:15 | CA Osasuna vs Atletico Madrid | 3.20 | 3.20 | 2.26 |
| 14. 29/01/23 | 18:45 | SC Cambuur vs Fortuna Sittard | 2.75 | 3.35 | 2.45 |
| 15. 29/01/23 | 19:30 | Bayer Leverkusen vs Borussia Dortmund | 2.46 | 3.50 | 2.65 |
| 16. 29/01/23 | 20:30 | RC Celta de Vigo vs Athletic Bilbao | 2.85 | 3.00 | 2.55 |
| 17. 29/01/23 | 21:00 | Boavista Porto vs Portimonense SC | 2.27 | 3.20 | 3.15 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 28/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 1482 | Accrington vs Leeds | 7.50 | 5.13 | 1.32 |
| 15:30 | 2389 | Walsall vs Leicester | 7.71 | 4.74 | 1.34 |
| 16:00 | 1116 | Kiyovu Sports vs APR FC | 2.75 | 2.80 | 2.64 |
| 16:00 | 1355 | Nchanga Rangers vs Chambishi FC | 2.26 | 2.74 | 3.42 |
| 16:00 | 1384 | Nkana FC vs Green Buffaloes | 2.23 | 2.65 | 3.64 |
| 16:00 | 1422 | Rwamagana City FC vs AS Kigali | 7.85 | 3.92 | 1.39 |
| 16:00 | 1491 | Nkwazi vs Kansanshi Dynamos | 2.50 | 2.50 | 3.32 |
| 16:00 | 2408 | Ankaragucu vs Gaziantep BB | 1.89 | 3.56 | 3.77 |
| 16:00 | 2999 | FC Muza vs Power Dynamos | 3.33 | 2.60 | 2.41 |
| 16:00 | 4081 | Red Arrows vs Kabwe Warriors | 1.90 | 2.81 | 4.58 |
| 16:00 | 4167 | Green Eagles vs Napsa Stars | 2.44 | 2.54 | 3.37 |
| 16:00 | 4714 | Cadiz CF vs Mallorca | 2.80 | 2.75 | 2.85 |
| 16:00 | 5349 | Lumwana Radiants vs Zesco United | 3.67 | 2.69 | 2.19 |
| 16:00 | 5971 | Prison Leopards vs Buildcon | 1.61 | 3.32 | 5.61 |
| 16:30 | 4505 | Mamelodi Sundowns vs Sekhukhune United | 1.41 | 4.24 | 7.42 |
| 17:00 | 1802 | Empoli vs Torino | 3.08 | 2.98 | 2.38 |
| 17:30 | 1402 | SC Freiburg vs Augsburg | 1.48 | 4.36 | 5.75 |
| 17:30 | 3092 | Mainz vs VfL Bochum | 1.66 | 3.86 | 4.55 |
| 17:30 | 3624 | Werder Bremen vs VfL Wolfsburg | 3.08 | 3.47 | 2.14 |
| 17:30 | 5287 | Hoffenheim vs Monchengladbach | 1.99 | 3.73 | 3.23 |
| 17:30 | 5681 | Hertha BSC vs Union Berlin | 3.37 | 3.12 | 2.16 |
| 18:00 | 1609 | Hull City vs QPR | 2.47 | 3.23 | 2.73 |
| 18:00 | 1775 | Coventry vs Huddersfield | 1.79 | 3.47 | 4.26 |
| 18:00 | 2152 | Fulham vs Sunderland | 1.44 | 4.51 | 5.89 |
| 18:00 | 2156 | Al Masry Club vs Farco FC | 1.68 | 3.39 | 5.38 |
| 18:00 | 2220 | Luton Town vs Grimsby | 1.42 | 4.43 | 6.50 |
| 18:00 | 2590 | Southampton vs Blackpool | 1.46 | 4.32 | 5.89 |
| 18:00 | 3350 | Blackburn vs Birmingham | 2.24 | 3.16 | 3.11 |
| 18:00 | 3395 | Sheffield Wed vs Fleetwood Town | 1.42 | 4.33 | 6.70 |
| 18:00 | 4696 | Middlesbrough vs Watford | 1.90 | 3.37 | 3.87 |
| 18:00 | 5105 | Ipswich vs Burnley | 3.10 | 3.30 | 2.18 |
| 18:00 | 5514 | Bristol City vs West Bromwich | 3.06 | 3.31 | 2.19 |
| 18:15 | 5849 | Girona vs Barcelona | 4.95 | 4.00 | 1.62 |
| 18:30 | 3134 | Moroka Swallows FC vs SuperSport Utd | 3.28 | 2.91 | 2.32 |
| 19:00 | 2807 | Mukura vs Rayon Sports FC | 2.90 | 2.90 | 2.22 |
| 19:00 | 2866 | Madagascar vs Mozambique | 2.36 | 2.85 | 3.40 |
| 19:00 | 4848 | Troyes vs Lens | 4.76 | 3.82 | 1.66 |
| 20:00 | 4579 | Cremonese vs Inter | 5.75 | 4.36 | 1.48 |
| 20:30 | 2530 | Bayern Munchen vs Eintracht Frankfurt | 1.30 | 5.75 | 7.34 |
| 20:30 | 4277 | Sevilla FC vs Elche | 1.51 | 3.99 | 6.39 |
| 21:00 | 2431 | Marumo Gallants FC vs Orlando Pirates | 3.38 | 2.95 | 2.25 |
| 21:00 | 4565 | Preston vs Tottenham | 7.72 | 4.95 | 1.33 |
| 22:00 | 2381 | Niger vs Ghana | 3.60 | 3.15 | 2.11 |
| 22:00 | 3304 | Heerenveen vs Vitesse Arnhem | 2.13 | 3.32 | 3.22 |
| 22:45 | 3808 | Atalanta vs Sampdoria | 1.31 | 4.97 | 8.55 |
| 22:45 | 4175 | Sporting Lisbon vs Porto | 3.10 | 3.15 | 2.18 |
| 23:00 | 2967 | AZ Alkmaar vs Utrecht | 1.68 | 3.76 | 4.55 |
| 23:00 | 4452 | Getafe vs Betis | 3.05 | 2.85 | 2.55 |
| 23:00 | 5320 | Manchester Utd vs Reading | 1.16 | 6.54 | 13.78 |
| 23:00 | 5801 | Marseille vs Monaco | 2.08 | 3.58 | 3.18 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KMC YAIVAA COPCO FA LEO, YAAHIDI KUFIKA HADI FAINALI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI leo ikijitupa kwenye Uwanja wa Uhuru kucheza mechi ya 32 bora ya Kombe la FA kuivaa Copco ya Mwanza, klabu ya KMC imetamba kushinda mechi hiyo, ikisema lengo lao msimu huu ni kufika fainali.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala amesema kuwa lengo hilo limewekwa kwa sababu maalum, kwani wakifika fainali wanaweza kabisa kushinda mechi ya mwisho na kutwaa ubingwa. "Tunawakaribisha Copco ya Mwanza, tunafahamu mechi iliyopita ya Ligi Kuu tulipoteza mabao 3-0 dhidi ya Namungo, tumeyaacha hayo na sasa akili yetu ipo sasa kwenye michuano hiyo kwa sababu tuna malengo yetu. Lengo letu ni kufika fainali, ni kitu ambacho kinawezekana kwa sababu mechi zote zipo ndani ya uwezo wetu. Baada ya kufika fainali sasa tutaangalia lengo la pili ambalo ni kutwaa ubingwa kwa ajili ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao," alisema Mwagala.

Timu nyingi za kati kwenye Ligi Kuu zimeonekana kuhamisha nguvu zao kwenye michuano hiyo, baada ya nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye Ligi Kuu kuonekana finyu, kwani klabu za Yanga, Simba, Azam na Singida United zikionekana kuzihitaji zaidi na vitendo.

Mbali na mechi hiyo, leo kuna itakayopigwa saa 10:00 jioni, timu ya New Dundee ya Dodoma, itakuwa kwenye Uwanja wa Jamhuri kuikaribisha African Sports kutoka Tanga, na kwenye Uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma, Mbeya Kwanza ambayo imeukimbia mkoa wa asili na kuweka makazi yake mkoani humo tangu ilivyokuwa Ligi Kuu msimu uliopita, itawakaribisha ndugu zao wa Mbeya City, Singida Big Stars yenyewe itakuwa kwenye Uwanja wa Liti, Singida kucheza dhidi ya Ruvu Shooting ya Pwani, huku Geita Gold nayo, ikiwa Uwanja wa Nyankumbu, Geita itaialika Nzega United.

Michuano hiyo itaendelea kesho ambapo mbali na mechi ya Yanga dhidi ya Rhino Rangers, kutakuwa na mitanange kadhaa, Mashujaa FC ikicheza dhidi ya Prisons kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Kagera Sugar dhidi ya KenGold, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera na Namungo itakuwa nyumbani, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa Lindi kucheza dhidi ya Ihefu.



Naibu Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwl. Julius Nyerere wa Taaluma, Utafiti na Ushauri, Prof. Richard Kangarawe, akishikilia kombe alilokabidhiwa juzi na Waziri wa Michezo wa chuo hicho, John Buberwa (kulia), kwenye sherehe ya kuwapongeza wanafunzi wanamichezo walioshiriki mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania (SHIMIVUTA) na kushinda medali nane, kushika nafasi ya 10 kitaifa kwenye michezo hiyo iliyofanyika Mwanza hivi karibuni. Kushoto ni Naibu Mkuu wa Utawala, Fedha na Mipango, Dk. Evaristo Haule. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Lazima tuwachape*

INATOKA UK 24

nafasi mbalimbali ikiwamo Mwenyekiti, wajumbe wa bodi nafasi mbili na wajumbe wa bodi nafasi nne.

Mwenyekiti atakayechanguliwa atakuwa na nafasi ya kuchagua wajumbe wawili na kufanya kufikia nane kwa mujibu wa kanuni ya klabu hiyo.

Wagombea waliopita katika nafasi ya mwenyekiti ni wawili ambao ni Advocate Mosses Kiluwa na Murtaza Mangungu anayetetea nafasi yake.

Wajumbe ni Seif Muba, Seleman Haroub, Idd Kitete, Issa Masoud, Abubakari Zebo, Abdallah Mgomba, Edward Mweladzi, Rashid Khamsini, Asha Baraka, Pendo Aidan na Aziz Mohamed.

Simba wanatarajiwa kufanya uchaguzi wao kesho Jumapili katika ukumbi wa kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), uliopo jijini Dar es Salaam.

## Doumbia tayari kuitumikia Yanga

INATOKA UK 24

uhitaji huo wa uharaka wa kumchezesha. Kwenye mchezo unaokuja dhidi ya Rhino Rangers, tunaweza kumuona akiwa anacheza."

Doumbia anakuwa ni mchezaji wa pili kutoka Mali kwenye klabu ya Yanga, wa kwanza akiwa ni golikipa namba moja wa timu hiyo, Djigui Diarra.

Pia anakuwa mchezaji wa tatu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kutoka nchini humo, kwani Simba ina mchezaji kutoka nchini humo, Sadio Kanoute.

Kamwe pia amewataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo hasa wakazi wa Dar es Salaam kuhudhuria mechi mbalimbali za timu hiyo inapocheza, kwani mahudhurio yao kwa sasa hayaridhishi.

"Ukiangalia mahudhurio kwenye mechi za nyumbani bado hayaridhishi, mwisho wa msimu tutakaa kufurahia pamoja tukiwa na mataji, lakini utajisikiaje wakati mwanachama au shabiki unashangilia, lakini haukuwa na mchango wowote?

"Ukiachana na kununua jezi, kununua vitu mbalimbali vya klabu pamoja na kutumia majukwaa ya mitandao ya kijamii ya klabu, moja kati ya jukumu kubwa la shabiki ni kwenda uwanjani na kuisapoti timu yake ikiwa inacheza," alisema Kamwe.

Michezo
Nipashe
Jumamosi Januari 28, 2023




**Benzema ataka mabao Real Madrid**

UKURASA 21



Wachezaji wa Simba, Shomari Kapombe (kushoto) na Kibu Denis wakijifua mazoezini. **PICHA: SIMBA**

## Doumbia tayari kuitumikia Yanga

**Na Adam Fungamwango**

BEKI mpya wa Yanga aliyesajiliwa mwishoni mwa dirisha dogo la usajili kutokea klabu ya Stade Malien ya nchini Mali, Mamadou Doumbia huenda kesho Jumapili akavaa jezi ya klabu hiyo kwa mara ya kwanza kwenye mchezo wa Kombe la FA hatua ya 32 bora, wakati timu hiyo itakapokipiga Rhino Rangers.

Mchezo huo wa Yanga dhidi ya Rhino Rangers kutoka Tabora inayoshiriki Ligi Daraja la Pili utapigwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema wanachama na mashabiki wa klabu hiyo wanaweza kumuona mchezaji huyo kwa mara ya kwanza kama benchi la ufundi litaona inafaa, ingawa wao kama uongozi wamesahakamilisha kila kitu.

"Sasa kilichobaki ni kwao tu ni benchi la ufundi, kwa upande wa uongozi taratibu zote za vibali zimekamilika.

"Kwanza kabisa benchi la ufundi lilitaka kumuona kwenye mazoezi, siku aliyofika ilikuwa ni usiku sana, kesho yake hakufanya mazoezi kwa sababu alikuwa amechoka na ilikuwa ni siku moja kabla ya mchezo na Ruvu Shooting, ndiyo maana hakucheza," alisema Kamwe.

Aliongeza; "pia alikuwa hajafanya mazoezi na timu, hajajua muundo wa timu, na ukiangali safu yetu ya ulinzi hatukuwa na

INAENDELEA UK 23

# Lazima tuwachape

## ●●● Ni Simba dhidi ya Coastal hatua ya 32 bora FA leo, makocha watoa tambo, Try Again ataka wanachama...

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Simba kinashuka dimbani leo katika mchezo wa hatua ya 32 bora ya Kombe la Shirikisho la mpira wa miguu Tanzania maarufu FA, kikiwakaribisha Coastal Union kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Simba inaingia kwenye mchezo huo huku ikiwa na habari njema ya kurejea kwa wachezaji wake majeruhi ambao sasa wako fiti akiwamo kinara wao wa mabao kwenye Ligi Kuu, Moses Phiri na beki Inonga Baka ambao jana walionekana wakifanya mazoezi na wenzao.**

Wekundu hao wa Msimbazi wanahitaji kupata matokeo ili kufuzu na kucheza katika hatua ya 16 bora katika michuano hiyo, kwani atakayefungwa leo anafungasha virago.

Kumbukumbu zinaonesha kwamba, Simba imekuwa na matokeo mazuri kila inapokutana na Coastal Union iwe nje au ndani ya uwanja huo wa Mkapa.

Coastal Union inahitaji kupata matokeo mazuri ili kusonga mbele baada ya msimu uliopita kutinga fainali kabla ya kufungwa na Yanga, mchezo uliopigwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, alisema wamejiandaa vizuri na wachezaji wake wako tayari kupambana kutafuta matokeo mazuri.

Alisema anafahamu uchezaji wa Coastal Union, lakini utakuwa mchezo mgumu na ushindani mkubwa kwa sababu ya hatua ambayo wanacheza kwani kila mmoja anahitaji ushindi.

"Kikosi kipo imara tuko tayari kwa mechi ya kesho (leo), naenda kucheza na timu yangu ya zamani, tumekuwa na matokeo mazuri mechi zilizopita tulipokutana nao, lakini tunacheza kwa kuwaheshimu na tahadhari kubwa ili kupata ushindi," alisema Mgunda ambaye ni kocha wa zamani wa Coastal.

Aliongeza; "mchezo huu ni mtoano na anayefungwa anaondolewa katika mashindano, lazima tushinde na wachezaji wetu wanafahamu hilo na tunaenda kutafuta ushindi na sio pointi."

Naye Kocha Msaidizi wa Coastal Union, Joseph Lazaro, alisema mchezo huo utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu ya uwepo kwa Mgunda ndani ya benchi la ufundi la Simba.

Alisema wanaenda kupambana kutafuta matokeo mazuri kwa sababu wanafahamu uchezaji na ubora wa Simba wanapokuwa uwanjani hasa wakisaka ushindi.

"Huu ni mchezo mgumu kwa kila timu, kwa sababu ni mechi ya kutafuta ushindi, tumejiandaa vizuri kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri, ila kuna ugumu mkubwa hasa tunaenda kucheza na timu ambayo kocha Mgunda alikuwa kocha wetu sasa yuko kwa wapinzani wetu," alisema Lazaro.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again', amewataka wanachama wa klabu hiyo kuchagua viongozi sahihi ambao watafanikisha malengo yao.

"Huu ni wakati mzuri wa mashabiki wa Simba kutumia vizuri haki yao ya uchaguzi kwa kutupatia viongozi imara na kuendeleza kauli mbiu yetu nguvu na umoja ili kufikia malengo ya klabu katika mtu wa kutupatia mataji," alisema mwenyekiti huyo.

Baada ya viongozi waliokuwapo sasa kumaliza muda wao wa uongozi, Simba inatarajia kufanya uchaguzi wa kuwania

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >